
UKURASA WA 3

**TPHPA** yaokoa chakula tani milioni moja kuzuia wadudu



UKURASA WA 4

**Mlinzi** aliyepiga kelele Mandojo akauawa, atiwa pingu na polisi



UKURASA WA 7

**Mpina** asisitiza atasema ukweli daima, atoa rai kwa mawaziri

UKURASA 22





# Nipashe

Jumatano Agosti 14, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581768

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US


# Vigogo CHADEMA: Tumepigwa na polisi


"Kuna baadhi ya viongozi huwa wanadhani kwa sababu ya vyeo vyao hatuwezi kuwashughulikia, sasa ninawaambia tutaendelea kuwashughulikia..."

**Kamishna Awadh Haji**



"Polisi walimrusha Lissu kwenye gari, walimpiga Joseph Mbilinyi 'Sugu' na Katibu Mkuu Mnyika na kuvunja miwani yake."

**Benson Kigaila**



"Ni jukumu la waandishi kutoa habari kwa umma kuhusu kila jambo linaloendelea, hivyo mwandishi hapaswi kukamatwa au kuadhibiwa kwa kufanya kazi hii."

**Deodatus Balile**



• **Kuanika** yaliyojiri selo Mbeya; polisi watamba hawatishwi na nyadhifa... *Uk. 2*

UKURASA 10

## Fisi wavamia bodaboda, waua wawili





Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akipokea hati za utambulisho kutoka kwa Balozi Mteule wa India nchini, Bishwap Dey, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Mtoto wa askofu adai kanisa fidia bilioni 3.7/-

UK. 3

**MICHEZO** **REKODI ZA NYOTA MPYA SIMBA** UK.24 **MAONI,** UK.6




Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Bara, Benson Kigaira, akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, kuhusu hali ya viongozi wa chama hicho. Kushoto ni Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa chama hicho, John Mrema. **PICHA: SABATO KASIKA**.

# Vigogo CHADEMA: Tumepigwa na polisi

**Na Waandishi Wetu**

VIONGOZI na wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) waliokuwa wanashikiliwa na Jeshi la Polisi katika vituo mbalimbali nchini wameachiwa, huku baadhi ya vigogo wa chama hicho wakidai kupigwa wakati wa kukamatwa.

Licha ya uamuzi huo, jeshi hilo limeendelea kuliweka Jiji la Mbeya chini ya ulinzi kwa lengo la kuhakikisha azma ya chama hicho kufanya maandamano na kongamano haifikiwi.

Chama hicho kilipanga kufanya maandamano na kongamano jijini Mbeya juzi, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani, lakini kukawa na zuio la polisi na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kwa maelezo kuwa matamko ya baadhi ya viongozi wa CHADEMA yaliashiria kutokea uvunjifu wa amani.

Hata hivyo, chama hicho kilikaidi zuio hilo, viongozi wake wakitangaza kuendelea na mchakato wa kufanya kongamano hilo, wakidai kuwa makatazo ya aina hiyo yanakiuka sheria za nchi.

Baada ya tamko la viongozi hao wa CHADEMA, jeshi hilo liliimarisha ulinzi katika maeneo mbalimbali ya jiji hilo, ikiwamo kwenye Uwanja wa Ruanda Nzovwe ambako kongamano hilo lilipangwa kufanyika.

Mbali na kuimarisha ulinzi huo, jeshi hilo lilikamata viongozi wote wa juu wa chama hicho wakiongozwa na Mwenyekiti Freeman Mbowe, Makamu Mwenyekiti Tundu Lissu, Katibu Mkuu John Mnyika, Mwenyekiti wa Baraza la Vijana (BAVICHA), John Pambalu na Mwenyekiti wa Kanda ya Nyasa, Joseph Mbilinyi, maarufu Sugu.

**WADAI KUPIGWA**

Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA Bara, Benson Kigaila, aliwaambia waandishi wa habari katika ofisi za Makao Makuu ya CHADEMA Dar es Saalam jana kuwa baadhi ya viongozi wao waliokuwa wakishikiliwa na kuachiwa jana asubuhi, walipigwa wakati wanakamatwa.

"Katibu Mkuu (Mnyika) na Mwenyekiti wa Kanda ya Nyasa (Sugu), hawa viongozi hawakukutwa wanatenda jinai yoyote, walikutwa Ofisi ya Kanda ya Nyasa, Mbeya.

"Kilichotokea, walianza kumkamata Makamu Mwenyekiti Bara (Lissu) kwa kumburuza na kumrusha katika gari, Katibu Mkuu alikwenda kuona kwanini wanamburuza.

"Kamanda wa Polisi ambaye ni Kamanda wa Operesheni na Mafunzo (Kamishna Awadh Haji) akamwita Katibu Mkuu, alipokwenda akamnyang'anya miwani, akaivunja mbele ya polisi.

"Kuivunja ilikuwa ishara kwamba piga huyu. Polisi wakaanza kumpiga. Walitangulia kumpiga Sugu, wamempiga Katibu Mkuu na kuwarusha katika magari na kuwasafirisha kuwapeleka walikojua wao," alidai Kigaila.

Kuhusu hali za afya zao, Naibu Katibu Mkuu Kigaila alisema kuwa baada ya viongozi wa chama hicho kufikishwa Dar es Salaam na kuachiwa huru baada ya kila mmoja kupelekwa nyumbani kwake, walikwenda hospitalini.

Hata hivyo, Kigaila alipoulizwa na waandishi wa habari kuhusu hospitali wanakotibiwa viongozi wao, alisema wataeleza wenyewe kupitia mkutano utakaoitishwa kesho - Alhamisi "kwa sababu baada ya kuachana polisi na kwa kuwa hawana simu, kukutana nao ni mpaka waende kwao baadaye".

Kigaila alisema kuwa leo, viongozi wakuu wa chama hicho watakutana kujadiliana na kwamba kesho watazungumza na waandishi wa habari kuhusu kinachofuata na hatua watakazochukua kutokana na kilichojiri baina yao na Jeshi la Polisi pamoja na Ofisi ya Msajili.

"Afya za viongozi mtazijua siku hiyo kwa kuwa leo (jana) wamekwenda hospitalini. Tangu wamekwenda huko hatujawa nao na hatujui vipimo vinasema nini. Kwa kuwa simu zao hawana, ziko polisi, kuwaona ni mpaka kuwafuata waliko," alisema.

Kigaila alibainisha kuwa hadi juzi walitangaza idadi waliokuwa wanashikiliwa polisi ilikuwa 443, lakini taarifa ya Jeshi la Polisi inaonesha ni watu 520 ambao wameachiwa bila masharti yoyote kama walivyosema.

Kuhusu dhamana yao, Kigaila alisema, "jana (juzi) ilipofika saa moja hadi saa mbili usiku, viongozi wetu wa Mbeya kupitia mawakili wetu waliambiwa dhamana ziko wazi, wapeleke wadhamini.

"Tuliwaambia madai yetu waachiwe bila masharti na kama wanadhani wanapaswa kudhaminiwa wapelekwe mahakamani.

"Umekamata watu 520, huna sababu yoyote unataka kuwaachia kwa kutaka wadhamini. Wakienda wanapewa masharti wawe wanaripoti kila baada ya wiki, unapelekaje watu 520 kuripoti?

"Tunaomba Watanzania tuunganishe nguvu, udikteta, uvunjaji katiba, uonevu tutaushinda kwa kusimama pamoja. Tusiache kazi ikawa ya watu fulani, kutotendwa haki mtu mmoja iwe ni kutotendwa haki sisi sote," Kigaila alisema.

Kiongozi huyo wa CHADEMA pia alisema baadhi ya wanachama wao bado wako Mbeya wakihangaika kutafuta nauli za kuwarejesha makwao kwa kuwa magari yaliyotumika awali yaliamriwa kuondolewa Mbeya.

Kigaila alidai kuwa polisi walifunga milango ya ofisi ya CHADEMA (Mbeya) na kuondoka na funguo na kila aliyefika ofisini huko alikamatwa.

Alidai kuwa juzi polisi walimchukua Katibu wa Kanda aliyekuwa Kituo Kikuu cha Polisi Mbeya, wakaenda naye katika ofisi hiyo kufanya upekuzi, lakini walipofika wakadai hawana funguo ndipo walipovunja milango.

"Tunawaambia polisi hiyo milango wakaitengeneze. Ukijua kulikoroga, lazima ujue na kulinywa. Walichukua simu sita, laptop (kompyuta mpakato) moja na vitu mbalimbali," alidai.

Kigaila alidai Jeshi la Polisi pia linaendelea kushikilia vifaa vya waandishi wa habari na kutaka viachiwe.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi usiku, Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi nchini, Kamishna wa Polisi (CP) Awadh Haji, alisema viongozi wote na wanachama wa CHADEMA waliokuwa wanashikiliwa katika vituo mbalimbali vya polisi waliachiwa juzi jioni.

Alisema walirejeshwa katika maeneo waliyokuwa wanatoka kwa kusindikizwa na Jeshi la Polisi, huku akisisitiza kuwa viongozi wengi wa chama hicho walikuwa wametoka mkoani Dar es Salaam.

Alionya viongozi wa vyama vya siasa kuhamasisha wafuasi wao kufanya vitendo vya uvunjifu wa amani; jeshi hilo litawashughulikia kwa mujibu wa sheria bila kujali nyadhifa zao.

"Kuna baadhi ya viongozi huwa wanadhani kwa sababu ya vyeo vyao hatuwezi kuwashughulikia, sasa ninawaambia kwamba tutaendelea kuwashughulikia kwa mujibu wa sheria za nchi," alisema Kamishna Awadh.

Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) na Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA TANZANIA) wamelaani tukio la waandishi watatu kukamatwa na polisi wakati wakitekeleza majukumu yao katika Ofisi za CHADEMA Kanda ya Nyasa iliyoko eneo la Kadege, jijini Mbeya.

Waandishi waliokamatwa ni Fadhili Kitundwa na Ramadhani Hamis wa Jambo TV na Francis Simba, Mpigapicha Mwanzo TV.

Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile, alisema kilichofaywa na polisi ni kinyume cha Ibara ya 18 ya Katiba ya nchi inayotoa haki ya watu kukusanya na kuchakata taarifa bila kujali mipaka ya nchi.

"Sambamba na Katiba, Kifungu cha 7(a) (b) na (c) cha Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016, kinatoa haki kwa waandishi wa habari kufanya kazi ya uandishi wa habari.

"Ni jukumu la waandishi kuhabarisha umma kuhusu kila jambo linaloendelea, hivyo mwandishi hapaswi kukamatwa au kuadhibiwa kwa kufanya kazi hii," alisema Balile.

Tamko la Bodi ya Uongozi ya MISA TANZANIA, lilieleza kuwa tukio hilo ni kinyume na Katiba, Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa na ni ukandamizaji wa waandishi wa habari.

"Ripoti ya Waandishi Wasio na Mipaka (RSF) 2024, imeitaja Tanzania kupiga hatua kubwa kwenye uhuru wa vyombo vya habari, uhuru wa kujieleza kwa ukanda wa nchi za Afrika Mashariki.

"Matukio ya kukamata waandishi wakiwa kazini yanaweka doa kwa nchi yetu, hivyo ni muhimu mamlaka zinazotekeleza wajibu wake kwa mujibu wa sheria zikachukua tahadhari zote muhimu kuhakikisha kila mmoja anatekeleza majukumu yake," inasomeka sehemu ya taarifa hiyo ya MISA TANZANIA.

***Imeandaliwa na Romana Mallya (DAR) na Nebart Msokwa (MBEYA)**

HABARI KITAIFA

# Mtoto wa Askofu adai kanisa fidia bilioni 3.7/-

**Na Ally Hengo**

MTOTO wa John Sepeku, Askofu Mkuu wa Kwanza wa Kanisa la Anglikana Tanzania, Bernado Sepeku, amefungua kesi mahakamani kulidai kanisa hilo Sh bilioni 3.7 kwa madai ya kutwaa eneo la shamba lake lenye ukubwa wa ekari 20.

Kesi hiyo imefunguliwa katika Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi, iko mbele ya Jaji Arafa Msafiri na ilitajwa jana kwa ajili ya kuanza kusikilizwa.

Hata hivyo, kesi hiyo iliahirishwa na Kaimu Msajili wa Mahakama hiyo, Sarah Buya, hadi Septemba 13, mwaka huu, ambapo Sepeku anatarajia kupeleka watu watatu kwa ajili ya kutoa Ushahidi.

Akiahirisha kesi hiyo ya madai, Buya alisema hatua hiyo imefikiwa baada ya Jaji Msafiri kuwapo katika majukumu mengine ya kikazi. Mawakili wa upande wa mdai, Deogratius Butawantemi na Gwamaka Nsekela toka Diakonus Company Advocate walikubaliana na wakili wa mdaiwa, Dennis Malamba, kupangwa kwa tarehe hiyo .

Katika kesi hiyo ya madai nambari 378/2024 amdai Sepeku amewasilisha madai ya fidia hiyo kufuatia kudai kanisa hilo la Anglikana kuchukua eneo la hekari ishirini lililopo Buza wilayani Temeke jijini Dar es Salaam ambalo awali alipewa na baba yake Askofu John Sepeku, baada ya kustaafu ambalo walidumu nalo kifamilia hadi hivi karibuni kanisa hilo lilipovamia na kuligawa kwa mwekezaji.

Licha ya madai hayo yaliyopingwa na upande wa mdaiwa, Sepeku anadai fidia nyingine ya Sh. milioni 493 kwa madai ya kuharibiwa mazao yake aliyoyapanda ndani ya eneo hilo.

Katika hati ya madai, Sepeku anadai kuwa mazao hayo yangeweza kumwingizia kiasi hicho cha fedha iwapo yasingeharibiwa na mwekezaji huyo.

Askofu Sepeku alikuwa Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana Tanzania baada ya kugawanywa kutoka lililokuwa Kanisa la Anglikana la Afrika Mashairiki mwaka 1970.

Kabla ya hapo, alikuwa Askofu wa iliyokuwa Dayosisi ya Zanzibar na Dar es Salaam akiwa Askofu Msaidizi na ilipotenganishwa na kuwa Dayosisi ya Dar es Salaam, alikuwa Askofu wake hadi mwaka 1983 alipofariki dunia.

Mwaka 1970 alichaguliwa kuwa Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana Tanzania na kuwa katika nafasi hiyo hadi mwaka 1978 alipojiuzulu kutokana na hali ya afya yake.

Nafasi yake ilichukuliwa na Askofu Mussa Kahurananga ambaye alikuwa Askofu wa Dayosisi ya Western Tanganyika, Kigoma ambaye alishika wadhifa huo kuanzia mwaka 1978 hadi 1983.

Wengine walioshika nafasi ya Askofu Mkuu na dayosisi zao na miaka kwenye mabano ni John Ramashani (Tanga, 1984 hadi 1998), Dk. Donald Mtetemela (Ruaha, 1998 -2007), Dk. Valentino Mokiwa (Dar es Salaam, 2008- 2013), Dk. Jacob Chimeledya (Mpwapwa, 2013- 2018) na Dk. Maimbo Mndolwa wa Tanga mwaka 2018 hadi sasa.




Rundo la taka likiwa limetelekezwa bila ya kuondolewa katika makutano ya barabara ya Bagamoyo na Mikocheni Viwandani, Dar es Salaam jana na kuhatarisha afya za wafanyabiashara wa eneo hilo na wateja wao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TPHPA yaokoa chakula tani mil.1 kudhibiti wadudu

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MAMLAKA ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA), imeokoa tani milioni 1.1 za chakula kwa kudhibiti maelfu ya wadudu waharibifu waliovamia mashamba ya wakulima katika msimu wa kilimo uliopita.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Prof. Joseph Ndunguru, alisema hayo wakati wa makabidhiano ya maabara ya kisasa ya kutengeneza viuatilifu vya kibaiolojia iliyopo katika Mji wa Kibaha kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni tatu.

Alisema wadudu waharibifu waliodhibitiwa katika msimu uliopita ni panya ambao walikuwa wamevamia zaidi ya ekari 358,895 kwenye mikoa tisa nchini.

Prof. Ndunguru alisema wadudu wengine waliodhibitiwa ni viwavijeshi pamoja na ndege aina ya kwelea kwelea milioni 80 ambao walikuwa wamevamia maeneo ya Mbarali, Ruvu, Mbeya na halmashauri 24 nchini.

Akipokea maabara hiyo, Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli alisema kukamilika kwa maabara hiyo kutasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la sumukuvu na kufanya Tanzania kuanza safari ya kuingia kwenye soko la kimataifa la chakula.

Mweli aliwataka TPHPA kutumia maabara hizo kutafiti viuatilifu hai ili kupunguza matumizi ya dawa zenye kemikali kwenye mimea.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka hiyo, Prof. Andrew Temu alimhakikishia Katibu Mkuu huyo kwamba maabara hiyo imekuja kwa wakati mwafaka na kwamba TPHPA imejipanga kupunguza matumizi ya dawa zenye kemikali.

Alisema uwapo wa maabara kama hizo unakwenda kusaidia na kupunguza uharibifu wa mimea, lakini pia utaongeza ufanisi kwenye maabara na kufungua masoko ya nje.

Prof. Temu alisema bodi hiyo inaangalia namna ya kuandaa vijarida kwa ajili ya kufundishia maofisa ugani ambao wanatumika na wakulima wa mazao mbalimbali hapa nchini.

## Janabi atoa ofa wagonjwa 10 wa figo kutibiwa bure

**Na Christina Mwakangale**

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi, ametoa ofa kwa wagonjwa 10 wa figo wanaohitaji kupandikizwa figo kujitokeza, ili kupatiwa huduma hiyo.

Prof. Janabi, amesema hatua hiyo ni baada ya hospitali hiyo kupokea fedha kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan na kwamba upandikizwaji huo, utafanyika mapema iwapo wachangiaji wa figo 10 pia watajitokeza.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Uchangiaji Viungo Duniani, Prof. Janabi alisema hiyo ni awamu ya pili ya watakaonufaika na fungu la rais, huku 12 tayari wamekwishapandikizwa.

"MNH imepokea fedha kwa ajili ya upandikizaji na tayari wagonjwa 12 wamenufaika na wasio na fedha kamili kwa ajili ya kupandikiza. MNH inatoa ofa kwa wagonjwa 10 ambao wanataka kupandikiza na wajiandikishe, ili wapandikizwe.

"Kwanza wachangiaji wajitokeze kuvunwa figo kwa ajili ya watu 10. Tanzania ni moja kati ya tisa ambazo zinafanya upandikizaji wa figo katika Afrika kwenye nchi 54. Tule mboga za majani na matunda kuepukia ugonjwa. Mnyama tembo anaishi miaka mingi kwa majani tu," alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Figo MNH, Dk. Jonathan Mngumi, alisema wanaume ni kundi linaloongoza katika kuwachangia figo wagonjwa wa figo, huku kati ya 102 waliochangia asilimia 70 ni jinsi hiyo.

Alisema wachangiaji figo hospitalini hapo ni walio na umri kuanzia miaka 21 hadi 70 na kwamba umri si kizuizi, huku vigezo vikiwa undugu unafikia hatua nne wakiwamo binamu.

"Waliochangia hapa nchini ambao ni 102 wote wako salama. Kuchangia figo ni salama. Wachangiaji wawe na undugu hadi wa nne na kabla ya hapo watathibitishwa ukaribu wao na mgonjwa kwa kupimwa vinasaba," alisema.

Pia alisema kabla ya upandikizaji ni lazima, kuwapo na nyaraka halali za kisheria na kisha kamati inayoshughulikia masuala ya figo huketi kwa ajili ya kupitisha ombi hilo.

"Mashine za MNH takribani 70 zinafanya uchujaji damu na kati ya hizo 14 zipo Mloganzila. Nchini asilimia saba ya watu wanaougua figo. Kusafisha figo ni gharama hufanyika angalau mara mbili na uchujaji damu kwa wanaougua figo, kwa mwezi ni takribani awamu 5,000," alisema.Pia alisema miongoni mwa sababu za ugonjwa huo ni presha ambayo ikizidi inaharibu figo, pia kisukari aina ya pili ambacho hutokana na mtindo wa maisha usiozingatia lishe, pamoja na matumizi mabaya ya dawa za maumivu.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA KUONESHA NIA YA UTOAJI WA HUDUMA ZA UWEKAJI MISIMBO KWENYE ZA MALI ZA KAMPUNI YA EACOP KUMBUKUMBU NA: 000000581**

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP LTD) inaalika kampuni au taasisi yenye uzoefu na sifa nzuri kuonyesha nia kwa ajili ya utoaji wa huduma za uwekaji misimbo kwenye mali za kampuni ya EACOP.

Kampuni ya EACOP inajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini la kusafirisha Mafuta linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
Wigo wa Huduma unajumuisha uundaji wa misimbo maalum inayokidhi mahitaji ya EACOP, ikionesha idadi na misimbo mahususi iliyoidhinishwa kwa kila mali ya EACOP katika Ofisi za EACOP nchini Tanzania. Huduma itakayotolewa itajumuisha.

- Uhakiki wa mali zilizopo kwa kulinganisha na mali zilizomo kwenye rejista kabla ya kuingizwa kwa misimbo maalum ya kielektroniki inayoweza kusomeka na Visoma Misimbo ya kielekitroniki (BCR) ambayo inapaswa kuonekana kwa urahisi kutoka umbali wa kawaida ikiwa na sifa zifuatavyo.
  - Malighafi itakayotumika; iwe ya kuvutia sana ya inchi 020" iliyopakwa rangi ya alumini kwa juu.
  - Tumia gundi ya kudumu ya 3M 467 inayostahimili msukumo (kanieneo) kwa upakaji wenye mgandamizo wa kudumu.
  - Nakala ya Lebo; Ubora wa juu, wa kudumu, na uwezo wa kustahimili hali mbaya ya hewa kati ya kiwango cha jotoridi ya 100C hadi 850C na isiyoyeyuka kirahisi, nyembamba, na yenye kunyumbulika vya kutosha kufikia maeno na hali mbalimbali.
  - Rangi: Michoro yenye rangi nyeusi nyuma ya muonekano wa rangi ya fedha.
  - Ukubwa: milimita 39 kwa milimita 13 (mm 39 x mm13).
  - Ufungashaji: Utolewa kwa mpangilio maalum, bila kukosa kwa asilimia mia (100%)
- Kifaa chake cha kusoma kadi kinapaswa pia kutolewa.

**MAELEZO YA ZIADA**
- Namba ya usajili ya Mali katika mfumo wa msimbo wa kielektroniki ili kuwezesha usomaji kwa skana.
- Neno 'The East African Crude Oil Pipeline' liwe kama linavyoonekana kwenye Nembo ya EACOP.
- Lebo za kwenye mali lazima ziwe na namba za kawaida pamoja na herufi ikijumuisha marejeleo ya kipekee kulingana na asili ya mli k.m. samani, vifaa nk.
- Lebo ya kwenye mali inapaswa pia kujumuisha mahali mali ilipo k.m. Ofisi ya Dar es salaam.

**MAHITAJI MHIMU:**
**Makampuni yanayoonesha nia yanatakiwa kutuma maombi kwa kuambatanisha nyaraka zifuatazo:**
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (**TRA**) na Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi kwa mwaka wa uliopo.
- Nakala ya ripoti rasmi ya ukaguzi ya hivi karibuni kutoka kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (**BRELA**).
- Cheti halali cha usajili na leseni ya biashara.
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamejisajili au wametuma maombi ya kujisajili na kuthibitishwa kwenye kanzidata ya EWURA (**LSSP**) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za Watoa Huduma wa Ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa kampuni za Ndani.
- Maelezo mafupi ya uzoefu, utaalamu na uwezo wa kutoa huduma zinazohitajika.
- Taarifa ya fedha kwa mwaka wa fedha uliopita na uthibitisho wa uwezo wa kifedha.
- Uwapo wa waafanyakazi wenye ujuzi (Sifa na uzoefu wa miaka lazima itolewe).
- Barua za uthibitisho na mapendekezo kutoka katika miradi iliyotekelezwa hapo awali kwa miaka 5 iliyopita.

Kampuni yenye nia, na uwezo wa rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hao juu yanapaswa kuonesha nia kwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwenda **cft.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) itumwe kabla ya **saa 11:00** jioni kwa saa za Afrika Mashariki (EAT) mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **29/08/2024** kichwa cha barua pepe kinapaswa kuwa: **EOI - 000000581 UTOAJI WA HUDUMA ZA UWEKAJI MISIMBO KWENYE MALI ZA KAMPUNI YA EACOP.**

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na kampuni yenye nia kulingana na tangazo hili la kuonesha nia na kufanya tathmini kwa kuzingatia vigezo vya ndani ili kubaini kampuni zitakazojumuishwa kwenye orodha ya kampuni ya awali yenye vigezo. Mwaliko wa kampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa kampuni ya awali yenye vigezo baada ya kampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD inaheshimu haki katika kufanya maamuzi ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.


# JKCI kufundisha waongoza watalii kumwokoa aliyeugua maradhi moyo

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) imesema inatarajia kutoa mafunzo kwa watoa huduma za utalii nchini, ili kujua namna ya kutoa huduma ya kwanza kwa mtalii atakayeugua ghafla akiwa nchini.

Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini ya JKCI, Prof. Mohamed Janabi aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumzia kongamano la wataalamu wapatao 1,000 wa moyo litakalofanyika Tanzania Aprili mwakani, zaidi ya nchi 40 za ndani na nje ya Afrika.

Alisema kongamnao hilo litakalofanyika Zanzibar, linalenga kutangaza utalii tiba kwa kusaidia utekelezaji lengo la serikali la kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2030, idadi ya watalii nchini ifikie milioni tano kwa mwaka.

"Kongamano hili linafanyika Zanzibar, dunia nzima itajua linafanyika wapi kwa sababu Zanzibar ni kati ya visiwa vizuri duniani. JKCI inachangia pato kuu la taifa kupitia tiba na tutatoa elimu namna ya kumhudumia mtalii au Mtanzania aliyeanguka ghafla.

"Tutatoa huduma kwa madereva, watoa huduma za hoteli na walioko kwenye Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) kwa sababu muda na kila dakika ni kitu muhimu katika kuokoa maisha ya mgonjwa," alisema Prof. Janabi.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge alisema kongamano hilo litajadili namna ya kutibu magonjwa ya moyo kwa kutumia teknolojia mpya ya akili mnemba (AI).

"Magonjwa ya moyo yanaongezeka kwa kasi duniani na watu wengi kupoteza maisha. Tumeona tuite wataalamu kutoka nchi mbalimbali. Tutajifunza namna ya kutibu kwa AI, hasa wagonjwa wenye kiharusi," alisema Dk. Kisenge.

Alisema utafiti mbalimbali utawasilishwa ili kubadilishana uzoefu huku wananchi wasio na taaluma ya utabibu wakifundishwa namna ya kuhudumia mtu aliyepata tatizo ghafla.

"Madaktari wengi watakaokuja hawatakuja tu kwa ajili ya kongamano, bali hata kwa kutalii. Hivyo, hii fursa kwa nchi katika kukuza uchumi," alisema Dk. Kisenge ambaye pia ni bingwa wa magonjwa ya moyo.

# Mlinzi aliyepiga kelele Man'dojo akauawa atiwa mbaroni na polisi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma linamshikilia Mlinzi Mkazi wa Nzuguni B, Raphael Ndamahnuwa (26), kwa mahojiano kuhusu tukio la kifo cha mwanamuziki wa Bongo Fleva, Joseph Michael, maarufu Man'dojo (46).

Man Dojo alifariki dunia akiwa anaendelea na matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma kutokana na kipigo alichopata baada ya kutuhumiwa kwa wizi akiwa eneo la Nzuguni B.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dodoma, Kaimu Kamanda wa Polisi, Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Polisi, Anania Amo, alisema mwili wa marehemu umehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhi maiti kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi na daktari ili kubaini chanzo cha kifo chake.

"Mnamo Agosti 11, mwaka huu, huko katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Joseph Michael, maarufu Man'dojo (46), mwanamuziki Mkazi wa Nzuguni B, alifariki dunia, akiwa anaendelea na matibabu," alisema Kaimu Kamanda Amo.

Alisema kifo chake kimesababishwa na kutuhumiwa kwa wizi baada ya kukutwa ndani ya uzio wa Kanisa Katoliki Parokia ya Watakatifu Wote lililoko Nzuguni B, huku akiwa amejificha katika banda la mbwa," alisema Kaimu Kamanda.

Alisema kuwa akiwa katika banda hilo, mlinzi wa eneo hilo alisikia mbwa wanabweka kwa nje ya kibanda chao na alipofika eneo hilo aligundua kulikuwa na mtu aliyejifungia ndani ya chumba kimojawapo cha banda hilo.

Kaimu Kamanda wa Polisi Amo alionya wananchi Mkoa wa Dodoma kujichukulia sheria mkononi kwa kuwa kufanya hivyo ni kinyume cha sheria za nchi.

"Niwasihi kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu kwenye vyombo husika ili wachukuliwe hatua stahiki," alisema Kaimu Kamanda.

Alisema kinachotakiwa ni kushirikiana na Jeshi la Polisi kuhakikisha wahalifu wote wanakamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Kaimu Kamanda Amo pia alisema jeshi hilo linaendelea na msako wa wahalifu kila kona huku wakisisitiza atakayebainika anafanya uhalifu atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Alisema kuwa kila siku jeshi hilo limekuwa linafanya msako wa kutafuta wahalifu na kuchukua hatua za kisheria pale wanapobainika kufanya makosa mbalimbali.



## Wenye ulemavu wataka ukaguzi utoaji ajira nchini

Na Elizabeth Zaya

CHAMA cha Watu Wenye Ulemavu Tanzania (CHAWATA) kimemwomba Kamishna wa Ajira nchini kukagua taasisi ambazo zinapaswa kuajiri watu wenye ulemavu na zitakazobainika kutofanya hivyo, viongozi wake wafikishwe mahakamani.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa chama hicho, Hamad Komboza wakati wa kongamano la watu wenye ulemavu, wadau wa maendeleo na madiwani kutoka Mkoa wa Dar es Salaam lililoandaliwa na Mbunge wa Viti Maalum kupitia kundi la Wenye Ulemavu, Stella Ikupa.

Komboza alisema suala hilo wamelipigia kelele kwa muda mrefu lakini linaonekana gumu kutekelezwa na taasisi nyingi za umma na binafsi.

"Hili limekuwa mfupa mgumu kutafunika, Sheria ya Ajira Na. 9 ya Mwaka 2010 inaelekeza kila penye ajira 20, asilimia tatu iwe ya watu wenye ulemavu, lakini ukichunguza katika taasisi na mashirika mbalimbali, hiyo haijafikiwa. Hili bado ni tatizo sugu," alisema Komboza.

Aliomba serikali kuwapatia bima ya afya bila malipo watu wenye ulemavu ili iwe rahisi kwao kupata huduma za matibabu tofauti na ilivyo sasa.

Mbunge kupitia kundi hilo, Stella, alisema licha ya kuwapo baadhi ya changamoto ambazo zinakumba watu wenye ulemavu, anatambua baadhi ya hatua ambazo tayari serikali imeanza kuchukua ikiwamo kuweka mpango wa kuwa na walimu wa kutosha wenye taaluma na uwezo wa kufundisha kundi hilo.

"Kwa mfano, suala la uchache wa walimu wenye taaluma na uwezo wa kufundisha kundi hili la wenye ulemavu, tayari serikali imeshaanza kulifanyia kazi kwa kuweka mikakati kuhakikisha vyuo vinafundisha lugha ya alama na elimu ya watu wenye uhitaji maalum.

"Si kwenye elimu pekee, tunaona hata kwenye maeneo mengine ikiwamo sekta ya afya. Kwahiyo, tushukuru kwa hatua hizi zinazochukuliwa na serikali, tunaamini kwamba itaendelea kufanyia kazi changamoto zetu zote, tuwe wavumilivu," alisema.

Stella alisema ataendelea kuzisemea changamoto zote za kundi hilo ili kuhakikisha zinapatiwa ufumbuzi.

Mkuu wa Idara ya Programu kutoka Taasisi ya Foundation for Civil Society (FCS), Nasir Rosai, alisema wao kama taasisi ambayo imekuwa ikiliwezesha kundi hilo, wanapendekeza kwamba katika kipindi hiki cha kuandaa Dira ya Taifa ya 2050, kuna haja kuzingatia mazingira wezeshi ya kidijiti kwa kundi hilo ambayo yatawasaidia kufanya uamuzi na kupata taarifa sahihi na kushiriki katika michakato ya maendeleo.

Alisema kuwawezesha katika mifumo mbalimbali ya kidijitali kutawasaidia pia kujiimarisha kiuchumi.

# 'Matibabu kwa mionzi yako chini Afrika'

Na Maulid Mmbaga

DAKTARI Bingwa wa Radiolojia (tiba mionzi), Lulu Fundikira amesema huduma ya uchunguzi wa tiba (MRI) barani Afrika iko chini katika matumizi na upatikanaji wake.

Kutokana na hali hiyo limeandaliwa kongamano la kisayansi litakalokutanisha wataalamu kutoka mataifa mbalimbali, ili kuongeza uelewa katika utoaji huduma.

Kongamano hilo limeandaliwa na Chama cha Kimataifa cha Matumizi ya Mionzi katika Tiba Kanda ya Afrika (ISMRM) na kamati ya matibabu ya mishipa ya fahamu Tanzania.

Kongamano hilo litakutanisha wataalamu wa radiolijia 250 kutoka Bara la Amerika, Ulaya, Asia na Afrika kwa lengo la kubadilishana uzoefu.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam Rais wa Chama cha Madaktari wa Radiolojia Tanzania (TARASO), Dk. Lulu, ambaye ni Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Muhimbili (MUHAS), alisema serikali imewekeza katika eneo la uchunguzi tiba, ikiwamo kufungwa mashine za MRI nne na kusaidia huduma hiyo kusambaa nchini.

Alisema kutokana na uwekezaji huo wameona kuna haja ya kuwezesha wataalamu waliomo nchini kuwa na uwezo zaidi wa kufanya matumizi mazuri na sahihi ya mashine hizo na kusaidia wananchi kupata huduma ya uchunguzi tiba ambayo ni ya uhakika zaidi.

"Hatua hiyo pia itasaidia matibabu kuwa mazuri na yatatolewa kwa wakati, na kongamano hili ambalo litakutanisha wanasayansi bingwa wa fani tofauti watafundishana kutokana na mawasilisho ya utafiti mbalimbali uliofanywa na itasaidia katika maeneo yetu kuona ni namna gani tutaweza kutumia MRI kusaidia watanzania," alisema Dk. Lulu.

Aliongeza kuwa kipimo cha MRI kina faida na ufanisi zaidi ya vipimo vingine vya mionzi ambavyo vinaweza kuleta madhara na kwamba huduma hiyo ina uwezo wa kuona magonjwa ambayo mashine nyingine za mionzi haziwezi kuyaona.

Alisema kipimo hicho kinaongeza thamani katika uchunguzi wa matibabu kwa mgonjwa na kufanya wataalamu kutoa majibu yatakayosaidia mgonjwa kupatiwa matibabu sahihi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya ISMRM, Dk. Mary Kamuzara, Bingwa wa Radiolojia, alisema kongamano hilo limeratibiwa na vyama vya wataalamu mbalimbali nchini, wakiwamo TARASO, wataalamu wa Radiolojia Tanzania (TARA), Wahandisi na Wateknolojia wa Vifaa Tiba Tanzania (AMETT), Shirikisho la Fizikia la Tiba Afrika (FAMPO), Baraza la Wataalamu wa Radiolojia (MRIPC) na Idara ya Huduma za Uchunguzi.

Alisema kongamano hilo la kimataifa la sayansi linatarajiwa kufanyika Dar es Salaam Septemba 19-20 mwaka huu na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.



Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis, akipanda moja kati ya miti 850 katika viwanja vya Msikate Tamaa, Kata ya Vingunguti, jijini Dar es Salaam juzi, iliyoandaliwa na Balozi wa Mazingira, Grit Mwimanzi (hayupo pichani), kwa ajili ya kutunza mazingira. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TAKUKURU yaokoa bilioni 1.6/- ukusanyaji mapato ya halmashauri

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Pwani imeokoa Sh. bilioni 1.6 kutoka vyanzo mbalimbali vya Halmashauri ya Mji wa Kibaha.

Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa huo, Ally Haji, aliyaeleza hayo jana mjini Kibaha wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu kazi zilizofanywa kwa kipindi cha Aprili hadi Juni mwaka huu.

Haji alisema walibaini hayo wakati wa ufuatiliaji makusanyo ya ushuru wa huduma mbalimbali, kwamba kuna viashiria vya uvunjifu wa maadili kwa kushindwa kuwajibika kwa baadhi ya watumishi.

"Katika ufuatiliaji tuligundua kuwa baadhi ya watumishi wa halmashauri kwenye kitengo cha ukusanyaji mapato wanashindwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za kukusanya Sh. bilioni 1.6 zilizokuwa zinapotea," alisema Haji.

Alisema TAKUKURU ilisaidia kuongeza makusanyo hayo baada ya kushirikiana na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha, ibaini mapato yaliyokusanywa awali kwa robo tatu za mwanzo kwa mwaka wa fedha 2023/24 ni kidogo kulinganisha na vyanzo vya mapato vilivyomo ndani ya halmashauri.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu kwa umma itolewe kuhusu kufanya kazi badala ya matambiko

**KATIKA** gazeti la Nipashe toleo la jana, kulikuwa na habari kwamba baadhi ya abiria wa treni inayopita katika Kijiji cha Katambile, Nsimbo mkoani Katavi, wanadaiwa kurusha sarafu katika Mto Ugala ulioko wilayani Nsimbo kwa imani ya kutatuliwa shida zao.

Imani kama hiyo si ngeni katika taifa la Tanzania kwa kuwa wengine wamekuwa wakienda kwenye mti mikubwa kama mibuyu kufanya matambiko na kuweka sadaka mbalimbali kama vile vyakula na fedha. Pia, wengine wamekuwa wakienda kwenye njia panda ya barabara au makutano ya njia na kuvunja nazi au kumwaga vyakula kwa imani kwamba watafanikiwa katika shida zao.

Kwenye Kijiji cha Katyambikwe, ambacho kinamaanisha kwamba, mtu anatakiwa akafanye matambiko, ambapo watu wanadaiwa kutupa sarafu za Sh. 50, 100, 200 na 500 kwenye mto uliopo sehemu hiyo. Baadhi ya wananchi na viongozi wa eneo hilo wamehojiwa na kuthibitisha kuwa jambo hilo ni la kweli na limekuwa likifanyika kwa muda mrefu.

Imebainishwa kwamba eneo hilo ambalo ni maarufu kwa jina la 'Tutani", treni inapofika mahali hapo, abiria wenye imani hiyo hurusha sarafu hizo kupitia mabehewa ya madirisha ikiwa ni njia ya kutimiza maelekezo ya waganga wao.

Jambo hilo linafanyika katika eneo la treni itokayo Tabora kwenda Mpanda mkoani Katavi, halina tofauti na maelekezo ya waganga hao kama ya kuweka vitu chini ya miti, kupeleka wanyama kama kuku na mbuzi kwa waganga ili kufanyiwa kafara.

Kwa mujibu wa mkazi mmoja wa Kijiji cha Katyambikwe, jambo hilo ni desturi kwa watu na limekuwapo enzi na enzi. Watu wanaokwenda kwa waganga wanaulizwa watapita njia gani watokapo huko na wanapo jibu watasafiri kwa treni, basi wanaelekezwa wakifika mtoni hapo, watupe sarafu za fedha za Kitanzania ili watoe sadaka huku wakiaminishwa kuwa watafanikiwa kwa kufanya hivyo.

Baadhi ya watu wanaofanya hivyo ni wakulima ambao wakati mwingine hubeba dawa zinazodaiwa kuwa zitawasaidia katika shughuli zao, hivyo wanapofika kwenye mto huo wanatakiwa kutoa sadaka ya fedha kwa kurusha sarafu kwenye mto. Watu hao wamekuwa wakifanya hivyo kwa imani kwamba wakitumia dawa ambayo katika baadhi ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini huitwa 'Ndimilo' (dawa ya kulimia), watapata mazao mengi.


Jambo la kujiuliza kwani ni zaidi ya miaka 60 tangu nchi ipate uhuru huku mamilioni ya watu wakiwa wamepata elimu na mafundisho ya kidini kuhusu mila potofu bado mambo kama hayo yanaendelea kutendeka. Bado wako Watanzania wanaoamini kwamba bila kufanya matambiko na kwenda kwa mganga kufanyiwa dawa hawawezi kufanikiwa.

Viongozi mbalimbali wa serikali na wa dini wamekuwa wakisisitiza kuwa ili mtu afanikiwe ni lazima atumie juhudi na maarifa na kwamba kazi halali pekee ndiyo itakayomfanya kufikia malengo yake. Elimu hii inapaswa kuendelea kutolewa na viongozi wanapokuwa majukwaani badala ya watu kuendekeza imani na mila potofu zilizopitwa na wakati.

Eneo la Katyambikwe linapaswa sasa kuangaliwa kwa jicho la pili kwa kuchukua hatua dhidi ya watu wanaotupa sarafu kwenye mto kwa imani za kishirikina kuwa wanapofanya hivyo watatatuliwa shida zao au kufanikiwa katika malengo yao.

Serikali kupitia vyombo vya ulinzi na usalama, haina budi kuweka ulinzi eneo hilo kwa sababu watu hao wanavunja sheria. Kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, fedha ni tunu ya taifa na kila mmoja ana wajibu wa kuilinda na kuitunza na mtu yeyote atakayeichezea fedha atachukuliwa hatua.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Restuta James

# Siasa zetu zilenge R4 za Rais Samia

**MJADALA** unaoendelea kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari wiki hii ni taarifa zilizopewa uzito kwenye magazeti ni kuhusu kusitishwa kwa maandamano ya CHADEMA, yaliyolenga kuadhimisha Siku ya Vijana Duniani.

CHADEMA ilipanga kufanya maandamano na kisha mkutano wa hadhara katika uwanja wa Ruanda Nzovwe, jijini Mbeya, Jumatatu wiki hii yaliyoshajihishwa na kauli za Mwenyekiti wa Baraza la Vijana (BAVICHA), John Pambalu, aliyewataka vijana wajitokeze kwa wingi kuamua hatima ya taifa lao.

Kiongozi huyo akiwataka vijana wawaige wenzao wa Kenya, ambao waliandamana kulishinikiza bunge lao lisipitishe sheria ya fedha ya mwaka 2024/25.

Baada ya kufuatilia vuta nikuvute baina ya chama hicho na polisi na madai ya viongozi wa juu wa chama hicho kushikiliwa kuanzia juzi, kuna mambo kadhaa yanayoibuka.

Mosi, Kenya waliandamana kwa hoja mahsusi ya kupinga muswada wa fedha, ambao uliwaunganisha na kuiwajibisha serikali yao. Kilichotokea Kenya baada ya Rais William Ruto, kukubaliana na waandamanaji hadi kuvunja baraza lake la mawaziri, ni fujo.

Kwa yeyote makini anayefuatilia siasa za majirani hao, atabaini kwamba waandamanaji wamefanya uharibifu usiopimika. Tuliofuatilia maandamano yale kuanzia hatua za awali, tuliona kijana akiwa amebeba siwa ya bunge la nchi hiyo mtaani.

Kadhalika jengo la bunge hilo liliharibiwa, majengo ya umma na mali nyingi zikichomwa moto.

Baada ya kauli za baadhi ya viongozi wa CHADEMA, polisi ambayo ina wajibu wa kulinda usalama wa raia na mali zake, wakasimama kwenye nafasi yao kuzuia fujo ambazo bila shaka zingeweza kuitumbukiza nchi kwenye hasara kubwa.

Tumeshuhudia kwenye maandamano ya majirani, majeruhi na vifo vikiripotiwa huku mamia ya wananchi wakipoteza mali. Nafikiri, Tanzania tunapaswa kujifunza namna bora ya kuilinda nchi yetu isifike huko. Tufanye mjadala, tushindane kwa hoja bila fujo wala kumizana; huku tukizingatia R4 za Rais Samia Suluhu Hassan, ambazo ni Maridhiano, Mabadiliko, Ustahamilivu na Kujenga Taifa Upya.

Siungi mkono chama chochote cha siasa kunyimwa kufanya mkutano, lakini sikubaliani kuwapo na vurugu za kisiasa. Nasema hivi kwa sababu, polisi walikuwa na sababu za kuzuia maandamano ili Tanzania isiwe kama Kenya ambayo hivi sasa imeshapata hasara kubwa kwa biashara na shughuli za uzalishaji za wananchi kuumizwa kwa kiasi kikubwa.

Kitendo cha Jeshi la Polisi kuwaachia huru wafuasi na viongozi wa CHADEMA ni kutimiza ustahamilivu na R4 za Rais Samia. Ni kwa sababu, kama waliokamatwa wiki hii wangekamatwa kipindi cha awamu ya tano leo wangekuwa wamefunguliwa kesi za uchochezi na wangekuwa mahabusu wakisubiri kupelekwa mahakamani.

Bila shaka, wanaofuatilia utekelezaji wa R4 za Rais Samia, watakubali kwamba hazimaanishi kuruhusu fujo. Aidha si kwa ajili ya kufanya siasa zinazolenga kuleta machafuko kwenye taifa ambalo limekuwa mfano wa kuigwa wa amani na utulivu barani Afrika na duniani pia.

Tukumbuke, Wakenya wameandamana kwa sababu waliyoiweka bayana kama kuikataa sheria ya fedha. Sababu hii iliungwa mkono wazi wazi na asilimia kubwa zaidi ya wananchi wasiofungamana na mirengo ya kisiasa, na zikakosa muafaka wa kitaifa. Tanzania hatujafika huko.

Hoja nyingi zinatatuliwa kwa majadiliano kwenye msingi wa R4 na kilichofanywa na polisi kuwakamata baadhi ya viongozi ni kuepusha uvunjifu wa amani. Dhana ya R4 ya Rais Samia imetumika kuwaachia bila kuwaumiza wala kuwafungulia kesi.

Ninachoweza kusema ni kwamba dhana hiyo haina maana ya kuruhusu fujo au 'uholela' wa kisiasa bali kushirikiana kuijenga nchi na kuwa na Tanzania inayoimarika kiuchumi na kidemokrasia.

## HABARI KITAIFA

### Mpina: Nitasema ukweli daima

**Na Alex Sayi,** MEATU

MBUNGE wa Kisesa, wilayani Meatu, mkoani Simiyu, Luhaga Mpina amesema atahahikikisha anasema ukweli wakati wote kama kinavyomhitaji kiapo chake huku akiwataka wabunge na mawaziri kuwa wakweli pale unapofanyika ubadhirifu kwa mustakabali wa taifa.


Mpina alitoa kauli hiyo juzi wakati wa mkutano wa hadhara na wakazi wa wilayani Meatu uliofanyika viwanja vya Mpina, kijiji na kata ya Mwandoya.

Akihutubia mamia ya wananchi na wakazi wa maeneo hayo, Mpina alisema hawezi kufumbia macho maovu yakifanyika na kuwa atasema ukweli kwa kuwa aliapa kusema ukweli na kuwatetea wananchi.

"Mimi ni mwakilishi wenu bungeni na niliapa kwa Biblia takatifu. Sasa siwezi kuona watu wanamhujumu Rais, nikae kimya, siwezi kuwa mbunge mnafiki na kuendelea kupongeza mama anaupiga mwingi wakati kuna watu wanahujumu nchi," alidai Mpina.

Kuhusu kusimamishwa kuhudhuria vikao vya Bunge, Mpina alisema hatua hiyo imemuumiza na kuwa tayari amepeleka shauri mahakamani kushtaki uongozi wa Bunge na kuwa katika shauri hilo anasimamiwa na mawakili 100 na linatarajiwa kuanzia kurindima kuanzia Agosti 28, mwaka huu.

Baadhi ya wakazi wa Lubiga, wilayani hapa, akiwamo Omary Malula, walisema jukumu la mbunge ni kueleza adha wanazokabiliana nazo na kumwomba aendelee kuwasemea Watanzania na wananchi wa Kisesa pale wasiposikika.





Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu), Ridhiwan Kikwete (kulia), akisalimiana na Mkuu wa Kitengo cha Rasilimali watu cha Benki ya NMB, Joanitha Rwegasira, alipotembelea banda la benki hiyo, katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Vijana Kimataifa, iliyofanyika kitaifa jijini Dodoma jana. Wengine ni baadhi ya wafanyakazi wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri apongeza mpango wa NMB kuajiri vijana

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imesema mpango maalumu wa kuajiri vijana uliobuniwa na Benki ya NMB unapaswa kuigwa na taasisi zingine kwa kuwa unatoa fursa zaidi kwa vijana wa kitanzania kutimiza ndoto zao.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete alipongeza mpango huo alipotembelea banda la NMB kwenye maonesho ya Kilele cha Siku ya Vijana Kimataifa yaliyofanyika jijini Dodoma.

Ridhiwani alitoa pongezi hizo baada ya kupokea taarifa ya mpango wa ndani ya benki hiyo kuhusu kundi la vijana, ikionesha kuwa tangu kubuniwa mpango huo, tayari NMB imeshaajiri vijana 100 katika kada tofauti.

"Tunawapongeza sana, ninaomba mwendelee na moyo huu wa kusaidia serikali katika kutimiza ndoto za vijana. Sisi serikali tunatambua mchango wenu hasa vijana wanaopitia kwenye programu zenu," alisema Ridhiwani.

Mkuu wa Idara ya Rasilimali Watu wa benki hiyo, Joanitha Mrengo alisema program hiyo inawalenga vijana waliohitimu vyuo vikuu ambao wanachukuliwa na kupewa mafunzo maalumu kazini kabla ya kuajiriwa na wengine wanarudi kujiajiri baada ya kupata ujuzi wa vitendo.

Mrengo alisema vijana wanaochukuliwa kwenye mafunzo hayo huchukua miaka miwili na kila anayepitia hapo anakuwa mtumishi mzuri, ikiwamo wanaojiajiri wenyewe katika sekta binafsi kwamba wanafanya vizuri pia katika shughuli zao.

Kwa mujibu wa meneja huyo, NMB Management Trainee Program, mbali na ajira, pia inasaidia kuibua vipaji kwa vijana wenye mawazo bunifu ambao wanahitaji kuendeleza ubunifu wao ili wajiajiri na kuzalisha ajira kwa wenzao.

Mpango huo unalenga vijana waliomaliza shahada wakiwa na ufaulu wa kuanzia GPA 3.8 na wenye umri usiozidi miaka 25 ambao huchukuliwa na kufanyiwa usaili. Kwa watakaokidhi vigezo, wanapewa mafunzo huku wengine wakipata fursa ya kuajiriwa moja kwa moja ndani ya benki.

Akizungumzia ushiriki wao kwenye kongamano la vijana, alisema wamekuwa wakishiriki mara nyingi kwa ajili ya kukutana na kundi hilo ili kulipata elimu huku akitangaza kuwa Agosti 19, 2024 dirisha la maombi kwa fursa hizo litafunguliwa, hivyo vijana waombe.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED





Regina Masatya akiwa katika moja ya miradi yake ya kilimo.. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TASAF ilivyookoa maisha ya mama, watoto wanne

**Na Julieth Mkireri,**
BAGAMOYO

NI miaka 10 imepita tangu Regina Masatya (49) aingizwe katika Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Mkazi huyo wa Mapinga, wilayani Bagamoyo aliingia katika mpango huo baada ya mumewe kumwachia familia ya watoto wanne katika nyumba ya kupanga ya vyumba viwili, akilipa Sh. 6,000 kwa mwezi.

Hata hivyo, Regina alishindwa kumudu kulipa kodi hiyo na kulazimika kuwa anachimba mitaro ya mabomba na kung'oa visiki katika mashamba ili apate kipato.

Anasimulia kwamba safari yake ya maisha ya Mapinga ilianza baada ya kutoka Kahama mwaka 2000 akiwa na mumewe na watoto wawili. Familia yao iliishi kwa furaha kwa kipindi cha miaka minane kabla ya kuingia katika maisha magumu.

Regina anasimulia kuwa baada ya mumewe kumwacha na kwenda kuanza maisha mapya katika eneo la Zinga, alipanga nyumba na kuishi na watoto wake wanne kwa kufanya vibarua vya kulima mashamba ili apate fedha ya kununulia chakula.

"Wakati mwingine familia ililazimika kupata mlo mmoja kwa siku pale nilipopata kibarua chenye malipo kidogo. Sikuwa nimezoea maisha ya shida lakini nikalazimika kuyazoea.

"Kuna siku fedha ninayopata ni ndogo haimudu kununua chakula cha milo mitatu, nikifanikiwa kukidhi mlo mmoja, ninasubiri watoto wote watoke shule ndipo tunakula," anasimulia.

Anasema kuwa katika kipindi chote hicho, amekuwa akifanya kazi ambazo nyingi jamii imezoea kuona zinafanywa na wanaume.

"Sitasahau nilivyofanya kazi ya kuchimba mtaro wa kuwekea mabomba ya maji, ilikuwa ni kazi ngumu kwangu lakini sikuwa na mbadala, nililazimika kufanya hivyo ili watoto wangu wapate chakula.

"Vibarua kwenye mashamba nilikuwa ninapata Sh. 10,000 hadi 15,000 kwa siku. Kuchimba mitaro pamoja na kazi hiyo kuwa ngumu, nilikuwa ninaambulia Sh. 21,000 kwa siku, lakini wakati mwingine malipo yanafanywa kulingana na urefu wa bomba.

"Si kazi za visiki na mitaro pekee, hata kuchoma mkaa nimefanya ili nipate fedha za kununulia chakula wanangu na kukidhi mahitaji yao ya shuleni.

"Pamoja na kufanya kazi zote hizo, nilikosa fedha ya kulipa kodi kwa miezi sita hadi pale Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa alipomtafuta mume wangu anisaidie kulipia kwa mwenye nyumba.

"Mwenye nyumba alitaka kunitoa katika nyumba yake baada ya kukaa kwa muda mrefu bila kulipa kodi, chakula nacho kuna wakati nilikwamа nikawa ninategemea misaada kutoka kwa majirani. Hiki ndicho kipindi kigumu zaidi nilichopitia mpaka kufikia hapa nilipo.

"Mwaka 2014, TASAF walinikuta niko kwenye kipindi kigumu nikiendelea kufanya kazi ngumu kujikwamua na umaskini, walinitembelea nyumbani, walinikuta nikiwa ninatoka kibaruani, haikuwa kazi ngumu kukubaliana na taarifa walizopewa kuhusu maisha yangu," Regina anasimulia.

Anasema kuwa baada ya kuingizwa katika mpango huo wa TASAF alinufaika kwa kupata ruzuku kila mwezi ambayo ilimsaidia kununua chakula na mahitaji ya shuleni ya wanawe.

Regina anasema alitumia sehemu ya ruzuku hiyo kufanya shughuli ndogo za ujasiriamali, ndani ya miaka 10, uchumi wake ukaimarika hatimaye kuwa miongoni mwa waliotoka katika mpango.

Anasema kuwa mwanzoni mwa mwaka huu alipatiwa ruzuku ya Sh. 500,000 baada ya kujitoa katika mpango na hapo ndipo alipojiendeleza kwa shughuli za kilimo kwa kukodi mashamba kwa ajili ya kilimo cha viazi na mpunga.

"Ruzuku za kila mwezi ziliniimarisha katika shughuli za kilimo, pia nimefanikiwa kununua kiwanja na sasa ninatafuta fedha kwa ajili ya kujenga, kupitia kilimo ninaamini nitafikia malengo niliyojiwekea," anasema.

Regina tayari amewasilisha maombi ya kupata jenereta kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kipindi cha kiangazi kwa uongozi wa TASAF uliotembelea miradi yake ya kilimo.

Mkurugenzi wa Uratibu TASAF, Haika Shayo, aliyemtembelea mnufaika huyo akiongozana na watendaji wengine wa mfuko huo, anasema wapo wanufaika wamekuwa na matokeo chanya kupitia ruzuku wanazopata.

Haika anasema mnufaika huyo ni kati ya wanufaika wa mpango katika Wilaya ya Bagamoyo ambao walitembelewa na watendaji hao kuona maendeleo ya utekelezaji wa mpango.

Anasema lengo lao ni kuona chochote kilichoanzishwa katika mpango kinakuwa endelevu kwa kuzingatia maelekezo yanayotolewa.

Akizungumzia walengwa ambao wameanza kutoka katika mpango huo, Haika anasema wapo ambao tayari wamejiimarisha na kupewa ruzuku kuendeleza miradi waliyoanzisha na kutoa nafasi kwa wengine kutoka kaya maskini kuingizwa katika mradi.

Mmoja wa wadau wa maendeleo, Nancy Kataraihya, anasema amefurahishwa na namna wanufaika walivyoonesha mafanikio ya mpango huku akitoa wito kwa vijiji vingine kuonesha mafanikio kwa walengwa.

Mratibu wa TASAF wa Pwani, Roseline Kimaro, anasema mkoa huo unaendeleza jukumu la kusimamia, kuratibu na kutekeleza kazi zilizopangwa kwa walengwa wa mpango.

Roseline anasema wanufaika wamekuwa na mabadiliko kimaisha kwa kubadilika kiuchumi kulinganishwa na kipindi wakati wanaingizwa katika mradi.

Kwa mujibu wa mratibu huyo, hadi kufikia Juni 2024, kaya 18,487 za wanufaika wa mpango mkoani Pwani zilikuwa zimehitimu. Kati yake, kaya 4,451 zilianza katika dirisha la Januari hadi Februari na baadaye kaya 13,939 kwa malipo ya mwezi Juni.

Anabainisha kuwa kaya zilizobaki katika mpango kwa sasa ni 31,679 kwa Mkoa wa Pwani.

Mratibu wa TASAF Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Jalala Sammatta, anasema kuna makundi mawili ambayo yametoka katika mpango; waliotoka baada ya ruzuku ya uzalishaji na waliotoka baada ya kufanyiwa tathmini ambapo wote waliingia katika mpango mwaka 2014.

## Stanbic yatoa elimu ya fedha

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Stanbic Tanzania imeendelea na mpango wake wa kutoa huduma ya stadi za awali ya elimu ya kifedha kwa wanafamilia hasa watoto na vijana.

Utoaji elimu hiyo umefanyika hivi karibuni katika tawi la benki hiyo eneo la Peninsula huko Masaki, Dar es Salaam.

Meneja wa Wateja Maalum wa Benki ya Stanbic Tanzania, Irene Bizere, alisema huduma hiyo imeanzishwa ili kuwapatia watoto ujuzi wa kifedha, ikiwamo njia mbalimbali za kutafuta fedha, matumizi sahihi ya fedha, utunzaji na akiba binafsi.

"Kwa kuwapatia watoto elimu ya fedha, Benki ya Stanbic Tanzania inatarajia kuwajengea nidhamu na uelewa wa kifedha unaohitajika katika utunzaji fedha kwa ujumla.

"Tunaamini kwamba ujuzi wa kifedha ni ujuzi muhimu wa maisha ambao unapaswa kukuzwa tangu umri mdogo," alisema.

Meneja huyo alisema kupitia mpango huo, wanalenga kuwezesha kizazi kijacho kuwa na maarifa na zana wanazohitaji kwa kufanya uamuzi sahihi wa kifedha.

"Tukio hili lilikuwa na aina mbalimbali za mafunzo shirikishi yaliyoimarisha dhana za kifedha ambazo watoto walikuwa wameelimishwa. Mojawapo ya stadi walizofundishwa vijana hao ni kupanga bajeti.

"Mafunzo yaliendeshwa kwa njia ya vitendo kupitia uigizaji namna bora ya utunzaji fedha," alisema meneja huyo na kuongeza kuwa mafunzo hayo yana faida nyingi ambazo watoto watakuwa nazo hadi umri wa mtu mzima.

**"Kwa kuwapatia watoto elimu ya fedha, Benki ya Stanbic Tanzania inatarajia kuwajengea nidhamu na uelewa wa kifedha unaohitajika katika utunzaji fedha kwa ujumla.**



# Wananchi waokoa uoto wa asili Chome

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

USHIRIKISHWAJI wa wananchi wanaoishi vijiji vilivyopo pembezoni mwa msitu asili wa Chome wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro umesaidia kulinda uoto wa asili kupitia mradi rafiki kwa mazingira.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Danstan Kitandula baada ya kukagua utekelezaji wa miradi ya uhifadhi wa mazingira unaofanywa na Mfuko wa Hifadhi ya Milima ya Tao la Mashariki (EAMCEF).

Kitandula, alisema miradi inayotekelezwa kwenye jamii hizo, imesaidia kupunguza uharibifu wa mazingira uliokuwa ukifanywa na wananchi hao baada ya kudhibiti.

Alisema miaka ya nyuma kulikuwa na matukio ya moto, uchimbaji wa madini katika msitu huo na kuchangia kwa kiasi kikubwa kuharibu uoto wa asili na mazingira ya eneo hilo.

"Kwa sasa kama tulivyoona uharibifu haupo na uoto wa asili unarejea na haya yamewezekana kwa kuwa wananchi wananufaika na miradi ambayo imeleta ahueni katika misitu yetu," alisema Naibu Waziri huyo na kuongeza:

"Wananchi wameshirikishwa kuanzisha vitalu vya miti ya asili ambavyo vimesaidia kurejesha uoto wa asili, ukifika kwenye misitu huwezi kuamini miaka iliyopita iliharibiwa na shughuli za kibinadamu."

Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko huo,Francis Sabuni, alisema wanafadhili miradi hiyo kwa jamii, kwa lengo la kulinda mazingira na kuhakikisha wananchi wanapata vyanzo mbadala ili kuwawezesha kiuchumi.

Hata hivyo, alisema mbali na miradi kupunguza uharibifu katika misitu, pia imesaidia kustawisha jamii.

Sabuni, alisema kwa sasa wengi wameanzisha miradi mingine ya ujasiriamali inayowasaidia kusomesha watoto na kuwainua kiuchumi.

"Miradi imesaidia misitu kuendelea kuwa salama na kustawi na maisha ya jamii yanayozunguka yameboreka," alisema Mkurugenzi huyo.

Alisema tangu mwaka 2006 EAMCEF, imekuwa ikitoa ruzuku kwa wananchi wanaopakana na hifadhi za mazingira asili zilizopo safu za Milima ya Tao la Mashariki, ikiwa ni njia mojawapo ya kuwashirikisha kwenye uhifadhi na ulinzi wa biaonuai hizo.

Alisema kwa mwaka mfuko huo, umekuwa ukitoa ruzuku ya Sh. bilioni moja kwa ajili ya Hifadhi za Mazingira Asili na utekelezaji wa miradi rafiki wa mazingira kwenye maeneo yanayopitiwa na safu za milima hiyo.

Awali Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Deusdedit Bwoyo, alisema tangu wananchi waanze kushirikishwa na kuwa na miradi hiyo, wameshuhudia mabadiliko makubwa katika misitu hiyo.

"Mfuko umefanya kazi nzuri kwa kuwa tumeshuhudia miradi mingi katika mikoa ya Morogoro, Iringa na Tanga. Pia, kutokana na wananchi kuwa na vipato, wamepunguza kwenda kuharibu misitu ya asili," alisema

## 'Wanasiasa acheni kuwadanganya wafugaji'

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

MJUMBE wa Mkutano Mkuu Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupitia Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Lenana Soipey Lenganasa, amekemea kauli za baadhi ya wanasiasa wanaowapotosha wananchi kuwa serikali inataka kuwapora ardhi wafugaji na kuwataka kuacha mara moja.

Lenganasa aliyasema hayo jana wakati akizungumza na jamii ya wafugaji wa Kijiji cha Lengasiti katika Kata ya Naisinyai kwenye ziara ya Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka.

"Jamii ya kifugaji isipotoshwe na wanasiasa uchwara wanaodanganya umma kuwa, serikali itawapora ardhi yenu na kugeuza kuwa mapori tengefu," alisema Lenganasa.

Alisema wanasiasa hao ni dhahiri kuwa wanagombanisha wafugaji na serikali kuwa haiwezi kuleta maendeleo ya sekta ya elimu, afya, nishati ya umeme, maji na barabara kwa lengo la kuwafukuza.

"Wafugaji tusisikilize kelele za wanasiasa uchwara, wanaopotosha jamii kuwa, maeneo ya makazi na ya ufugaji yatageuzwa kuwa mapori tengefu," alisema Lenganasa.

Alitoa mfano wa eneo la milima ya Laletema kuwa kwenye ramani ya miaka iliyopita inatambulika kuwa ni pori tengefu, lakini wafugaji wanalitumia kwa malisho ya mifugo na shughuli nyingine, hivyo wasikubali kupotoshwa.

Alisema serikali inawapenda wafugaji ndio sababu imekuwa ikiendelea kuwaletea maendeleo katika maeneo yao, hivyo wanapaswa kuendelea kuiamini serikali.





Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Mwanga Hakika, Ridhuan Mringo (kulia), Makamu Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Raymond Tarimo (katikati) na Mjumbe wa Bodi, John Msemo, wakiwa katika Mkutano Mkuu wa Nne wa Wanahisa wa benki hiyo, uliofanyika wilayani Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro mwishoni mwa wiki iliyopita. Mkutano huo, ulijadili maendeleo ya benki hiyo na kuhudhuriwa na wanahisa zaidi ya 5,000. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Diwani asimikwa kuongoza Wamasai

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

DIWANI wa Kata ya Naisinyai wilayani hapa Mkoa wa Manyara, Taiko Laizer amesimikwa kuwa kiongozi wa kimila wa jamii ya wafugaji ya Wamasai (Laigwanani).

Diwani huyo, alisimikwa juzi kushika wadhifa huo na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Manyara, Peter Toima

Taiko, akizungumza baada ya kusimikwa kuwa kiongozi wa kimila na Toima ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye shughuli hiyo iliyohudhuriwa na wageni mbalimbali kutoka mikoa ya Manyara, Arusha na Kilimanjaro, aliahidi kutenda haki bila kumuonea mtu yeyote.

"Nawashukuru watu wote mliohudhuria kwenye sherehe hii, ndugu zangu na wake wangu kwa kunipa joto wakati nasimikwa kwangu kuwa kiongozi wa kimila," alisema Taiko.

Toima, alimpongeza Taiko kwa kuwa kiongozi wa kimila na kumtaka kuendelea kuwatumikia wananchi kwa uadilifu, imani na upendo.

Aliwataka wakazi wa eneo hilo kujitokeza katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika baadaye mwaka huu na kuwachagua wagombea wa chama hicho.

Mbunge wa Kiteto, Edward Ole Lekaita, alimpongeza diwani huyo kwa kusimikwa kuwa kiongozi wa kimila, huku akiendelea kuitumikia jamii yake kwa nafasi ya udiwani.

"Pamoja na salamu kutoka kwa majirani zenu wa Kiteto, tunaendelea kuishukuru serikali chini ya uongozi wa Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa namna inavyotekeleza miradi ya maendeleo,"alisema,

Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, alimpongeza diwani huyo kwa kusimikwa kuwa kiongozi wa kimila wa jamii hiyo ya wafugaji.

"Tunakupongeza ndio maana wafugaji wa Manyara, Arusha na Kilimanjaro kwa umoja wetu tumekusanyika hapa na tunaahidi kumlipia fomu ya kugombea urais mwaka 2025, Rais Samia," alisema Ole Sendeka.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Simanjiro, Kiria Laizer, alisema anatarajia viongozi wa kimila watawasaidia kukemea uuzaji holela wa ardhi kwa kuwa wanaushawishi katika jamii.

"Wengi ni wakubwa zangu siwafundishi kuongoza ila kupitia nyie mtaweza kuwasimamia viongozi wa vijiji na vitongoji wasiuze ardhi au kusababisha migogoro,"alisema Kiria.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Baraka Kanunga, alisema wataendelea kutoa ushirikiano kwa diwani huyo baada ya kuongezewa majukumu ya kuwa kiongozi wa kimila.



# Fisi wavamia bodaboda, waua wawili

## Umeme waua mafundi wakihamisha nguzo

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKULIMA na abiria wake, wamekufa papo hapo kwa kushambuliwa na fisi wakati wakisafiri kwa pikipiki kutoka kijiji kimoja kwenda kingine.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilibrod Mutafungwa jana alisema kuwa tukio hilo lilitokea Agosti 11, mwaka huu majira ya alfajiri katika Kijiji cha Kabusulu Kata ya Nyamatongo wilayani Sengerema.

Mutafungwa, alisema katika tukio hilo, Mkulima huyo, Devis Thomas (48), Mkazi wa Karumo akiwa anaendesha pikipiki aina ya SANLG kutoka Kijiji cha Igalagalilo kuelekea Kijiji cha Kilumo, amempakiza abiria huyo, Yohana Andrew (20), walivamiwa na fisi na kushambuliwa sehemu za miili yao na kufa papo hapo.

Alisema miili ya marehemu hao imefanyiwa uchunguzi wa kitaalamu na kukabidhiwa ndugu kwa ajili ya kufanya taratibu za mazishi.

"Polisi kwa kushirikiana na wananchi wa Kata ya Nyamatongo na Mamlaka ya Wanyamapori tumeanza msako wa kuwatafuta fisi hao ili wasiendelee kuleta madhara zaidi kwa wananchi," alisema Mutafungwa. Akizungumzia tukio jingine, Kamanda huyo, alisema mafundi umeme wawili wa Kampuni ya Man Electrical Engineering wamekufa papo hapo na wengine wawili kujeruhiwa kwa kupigwa 'shoti' wakati wakihamisha nguzo ya umeme kupisha ujenzi wa mradi wa barabara.

Mutafungwa, alisema tukio hilo lilitokea Agosti 10, mwaka huu, majira ya mchana katika Mtaa wa Semba Kata ya Lwanhima Wilaya ya Nyamagana.

"Tulipata taarifa mafundi umeme wa Kampuni iitwayo Man Electrical Engineering wakiwa wanahamisha nguzo za umeme kupisha mradi wa ujenzi wa Barabara ya Buhongwa kuelekea Igoma kupitia Kishiri walipigwa na mshituko wa umeme na kusababisha vifo vya watu wawili," alisema.

Aliwataja waliokufa kuwa ni Luhogo John (23), Mkazi wa Sengerema, Andolile Joseph (32), Mkazi wa Nyegezi,waliojeruhiwa kibarua, Samwel Malugu (23) na fundi, Frank Willium (23).

Alisema majeruhi hao walipatiwa matibabu katika Zahanati ya Buhongwa na kuruhusiwa kutoka baada ya hali zao kuendelea vizuri.

Kwa mujibu wa Mutafungwa, polisi wanawashikilia Mkandarasi wa kampuni hiyo, Fikiri Masinde (47) na fundi umeme, Charles Stephano (32) kwa tuhuma za uzembe kwa kushindwa kuwapa vifaa na maelekezo sahihi ya kazi mafundi hao ili kunusuru maisha yao.



Askofu wa Jimbo Katoliki la Shinyanga, Liberatus Sangu akiteta jambo na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, alipofika ofisini kwake, jijini humo jana kwa ajili ya kutoa taarifa za mwaliko wa sherehe za uzinduzi wa jimbo jipya la Kanisa Katoliki wilayani Bariadi mkoani Simiyu, zinazotarajiwa kufanyika hivi karibuni. **PICHA: VITUS AUDAX**

# UWT wakunwa kasi upanuzi wa bandari

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

UMOJA wa Wanawake Taifa (UWT) wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) umeihimiza Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) Kanda ya Ziwa kuhakikisha mradi wa ujenzi wa upanuzi na maboresho ya Bandari ya Mwanza Kaskazini unakamilika mwaka huu.

Mwenyekiti wa umoja huo, Mary Chatanda alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ziara yake ya kukagua ujenzi wa mradi huo unaotarajiwa kukamilika Novemba mwaka huu.

"Nimekagua mradi huu, ambao Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ametoa Sh. bilioni 18.6 kwa ajili ya ujenzi wa ghati, nimeona kazi inayofanyika ni nzuri pamoja na kwamba mradi ulipata changamoto kidogo umechelewa kukamilika kwa wakati, " alisema Chatanda.

Alisema kikubwa alichowashauri TPA na mkandarasi wa ujenzi huo kutoka kampuni ya nchini China aongeze kasi ya ujenzi ili ukamilike kwa wakati kulingana na mkataba.

Alisema endapo ujenzi wa ghati hilo ukikamilika kwa wakati, meli kubwa ya abiria na mizigo itatia nanga na kutoa huduma kwa wananchi.

Chatanda, alisema wana Mwanza wana kila sababu ya kujivunia kazi anayoifanya Rais Samia kwa sababu lengo lake kubwa ni kuboresha maisha yao na kuwarahisishia usafiri.

Kwa upande mwingine, kiongozi huyo aliwakumbusha wananchi kujitokeza kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapiga kura ili washiriki kikamilifu kuchagua viongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa baadaye mwaka huu na mkuu 2025.

# Wanaoficha watoto wenye ulemavu waonywa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge wa uhuru kitaifa Godfrey Mnzava, amewaonya wazazi kuacha tabia ya kuwaficha watoto wenye ulemavu majumbani na kuwapeleka shuleni kupata haki yao ya msingi ya elimu.

Mzava alitoa onyo hilo juzi wakati akiweka jiwe la msingi katika bweni la watoto wenye mahitaji maalum la Shule ya Msingi Iselamagazi.

Aliwataka kutumia fursa ya miundombinu iliyopo kuhakikisha watoto hao wanapata elimu bora kama wengine.

Akiweka jiwe la msingi kwenye ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika Shule ya Msingi Shilabela wilayani hapa alionesha kufurahishwa na halmashauri hiyo kutumia fedha za mapato ya ndani, na siyo kutegemea serikali kuu kama ilivyozoeleka kwa halmashauri zote nchini.

Aliwasisitiza kuendelee kutenga fedha hizo ili kutekeleza miradi mbalimbali, ikiwamo na kukamilisha maboma ambayo yalianzishwa kujengwa kwa nguvu za wananchi.

Mbunge wa Solwa, Ahmed Salum, aliwasisitiza wazazi na walezi jimboni humo kuwapeleka shuleni watoto wenye uhitaji wakapate elimu kama wengine kwa kuwa ni haki yao ya msingi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Dk. Kalekwa Kasanga, alisema Mwenge huo katika halmashauri hiyo, utakimbizwa umbali wa kilomita 160 na kupitia miradi 14 ya maendeleo yenye thamani ya Sh. bilioni 1.7.

# Halmashauri zatakiwa kushirikiana

**Na Restuta Damian,** KAGERA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa (ALAT) Taifa, Murshid Ngeze amezitaka halmashauri nchini kushirikiana kwenye utendaji kazi ili kuleta maendeleo nchini.

Ngeze alitoa wito huo juzi wakati akizungumza na viongozi na watendaji wa halmashauri mkoani hapa.

Alisema ushirikiano ni msingi wa mafanikio ya maendeleo ya jamii kupitia miradi katika maeneo yao.

Alisema halmashauri zinatakiwa kushirikiana ili kutatua kwa pamoja migogoro na kujadiliana changamoto wanazokumbana nazo kabla viongozi wa kitaifa hawajafikia katika maeneo yao na kubaini udhaifu.

Ngeze, alisema usimamizi wa miradi unahitaji ushirikiano kati ya wataalamu, viongozi na wananchi ili kukamilisha kwa wakati.

Alisema kumekuwa na matatizo ya utozaji wa ushuru katika halmashauri na kuwa kero kwa wananchi wanapokuwa wanapishana kulipia.

Alitaka kuandaliwa kwa sheria ndogo za kusimamia utozaji ushuru na kupelekwa kwa wananchi ili zifanyiwe utekelezaji.

Vilevile, alitahadharisha kuwa suala la ushuru halitakiwi kuwa chonganishi baina ya serikali na wananchi kwani wanaotunga na kuondoa sheria ndogondogo ni wao kama halmashauri.

Baadhi ya viongozi wa halmashauri hizo waliahidi kusimamia kwa ushirikiano utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili halmashauri zote ziongee lugha moja kisheria.

Ukurasa 12



**Harakati kusafisha wamachinga, daladala zinahitajika tena Mbezi**

Ukurasa 14



**SAMBI KATIKA MIKONO YA WASIOMTAKIA MEMA**



# Jopo la wanasheria wa kampeni ya Samia walivyomtoa gerezani aliyebambikwa kesi

**Na Elizabeth Zaya**

HUDUMA ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, inayotetea wananchi na kuwapa haki pale inapokataliwa au kupindishwa, imewagusa wengi wanaolalamikia migogoro ya mirathi na ardhi, lakini yuko mtu imemtoa gerezani, alikofungwa akidai alibambikiwa kesi.

Ni Rajabu Chisonga(29), anayeishi kijiji cha Machemba Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, aliyetolewa jela kwa msaada wa jopo la wasaidizi wa kisheria wa Msaada wa Kisheria ya Mama Samia.





Viongozi wakishuhudia uzinduzi wa kampeni Msaada wa Kisheria wa Mama Samia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Akizungumza na Nipashe kwenye maonyesho ya Nanenane hivi karibuni, Kisonga anasema mwishoni mwa 2022 akiwa kazini kujitafutia riziki yake na wazazi wake, alikamatwa na kundi la watu wakijiita polisi jamii, waliompeleka kituo cha polisi wakidai anavuta bangi.

"Baada ya kukamatwa nilikosa wa kunitetea, nikapelekwa mahakamani na kufungwa jela. Nilia sana kwa sababu ndiye mlezi pekee wa wazazi wangu, baba ni kipofu na mama yangu hana nguvu ya kufanya shughuli yoyote ya kujitafutia kipato."

Anasema: " Ndiye tegemeo lao, kwa hiyo baada ya hukumu sikujiwazia, niliwaza kuhusu wazazi wangu. Nililia sana na kujitetea kwa nguvu lakini sikusikilizwa."

Anakumbusha kuwa alikamatwa akiwa kazini akifyatua matofali kwa ajili yake na wazazi wake.

Anasema Mei mwaka jana alikutanishwa na jopo la Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia ambao baada ya kuzungumza naye gerezani liliahidi kufuatilia.

"Baada ya hapo walianza kufuatilia hatua moja baada ya nyingine, mahakama ikabaini kwamba nilikamatwa kimakosa na Agosti 7 mwaka jana nikaachiwa huru.

"Kwa kweli niwashukuru sana wanasheria wa kampeni ya Mama Samia, wamenisaidia niungane na wazazi wangu tena. Maana miaka miwili wazazi wangu kuishi bila mtu wa kuwasaidia sijui ingekuwaje," anasema Kisonga.

Mtendaji wa Kijiji cha Machemba, Ally Chapuma, anasema chanzo jopo la wanasheria hao kuamua kumsaidia kijana huyo kilianzia kwa wananchi kupiga kelele wakitaka aachiwe huru.

Tangu mwanzo waliamini kwamba hakustahili hukumu kwa sababu hakuwa mhalifu licha ya kwamba alihukumiwa kifungo.

"Huyu kijana tumeishi naye hana historia ya uhalifu na usingeweza kumkuta kwenye makundi ya ovyo, alikuwa anahangaika na vibarua kwa ajili ya kuhudumia wazazi wake, kwa hiyo tulishangaa kusikia amekamatwa anavuta bangi,"anasema Chisonga.

"Kwa hiyo siku wanasheria walipofika hapa, wanakijiji walipiga kelele, wakaomba asaidiwe kwa kuwa hakutendewa haki na wanamfahamu ni raia mwema na wazazi wake wanamhitaji."

Mwenyekiti wa kijiji anashukuru jopo hilo la msaada wa kisheria kwa kuwasikiliza, kulibeba na kufuatilia suala hilo mpaka alipoachwa huru na sasa anaendelea na shughuli zake na kuhudumia wazazi wake.

Ofisa Uchunguzi Mkuu, Huduma za Msaada wa Kisheria kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Laurent Burilo, anasema baada ya kufikishiwa ombi hilo kwa wananchi waliamua kufuatilia kwa kutumia njia mbalimbali za kisheria na kubaini kwamba kijana huyo hakustahili kuwa gerezani.

"Na tulibaini kwamba alikuwa kijana aliyekuwa anategemewa na wazazi wake ambao hawajiwezi. Kwa hiyo baada ya jitihada za kisheria kupitia jopo letu, na mazungumzo marefu mahakama ikasema kufikia Agosti mwaka jana itamwachia huru."

Kwa mujibu wa Burilo, Kisonga alihukumiwa kutumikia kifungo cha miaka miwili katika Gereza la Wilaya ya Tunduru.

Burilo anasema baadhi ya visa ni pamoja na baadhi ya ndugu kufarakana na wengine kutishiana kuuana kutokana na migogoro inayotokea kwenye familia zao.

Anasema si kwa familia, ipo inayohusisha majirani au taasisi za umma na wananchi ambayo inafikia wakati husababisha mfarakano na kuhatarisha amani.

Anatoa mfano mgogoro wa ndugu ambao ulidumu kwa zaidi ya miaka 10, wakigombania kipande cha ardhi walichogawiwa na baba yao mzazi na wamekuwa hawasalimiani na wakati mwingine kutishiana kuuana.

Anasema walipatanishwa na timu ya Mama Samia Legal Aid Campaign na sasa wana amani.

Anasema tangu kuzinduliwa kwa kampeni hiyo mwaka jana, wananchi zaidi ya 500,000 wametatuliwa migogoro yao kwa njia ya kisheria katika mikoa ambayo wamewafikia hadi sasa.

Kampeni hiyo ambayo imekuwa ikizunguka katika mikoa mbalimbali tangu ilipozinduliwa mwaka jana, inafika hadi katika maonesho mbalimbali ikiwamo ya Sabasaba na sasa iko katika maonesho Nanenane Dodoma.

Wananchi wengine waliofika katika maonesho ya Nanenane wamesimulia namna walivyosaidiwa matatizo yao kupitia kampeni hiyo.

Lameck Kipiliango, anasema kwa kipindi kifupi ambacho kampeni hiyo imefanya kazi imewasaidia watu wengi ambao walipoteza matumaini hasa wale wasio na uwezo wa kifedha kulipia gharama za mawakili.

Kipiliango anasema ni miongoni mwa walioteseka kwa muda mrefu kutafuta haki katika eneo la ardhi lakini kwa sababu ya kutokuwa na fedha alikata tamaa.

"Nimefurahi nimepata msaada wa kisheria katika ardhi yangu niliyoihangaika siku nyingi, ni Mungu aliniongoza ni je hapa, tunamshukuru sana Mama Samia ameleta kitu kipya huko nyuma hakikuwapo," anasema Kipiliango.

"Ila kama ingempendeza Rais Samia, hii isiishie kuwa kampeni maana yenyewe huwa ikifika kip-

INAENDELEA UK. 12

# Harakati kusafisha wamachinga, daladala zinahitajika tena Mbezi

## •Trafiki, TANROADS waingilia kati



Foleni na vurumai za wafanyabiashara wadogo Mbezi Mwisho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**NA MWANDISHI WETU**

MWAKA jana karibu miji na majiji yote yalishuhudia juhudi za serikali kusafisha vituo vya mabasi na barabara ili kuwa na miji inayopendeza na kuondokana na usumbufu, msongomano na uchafu unaosababishwa na biashara za wamachinga.

Ilikuwa kero inayochanganyikana na hofu ya kuumizwa kwenye ajali za barabarani kutokana na wamachinga kuzingira kila eneo na kupanga bidhaa hadi kando ya barabara kuu na zile za 'stendi'.

Mathalani Dar es Salaam, askari na wanamgambo wa jiji walisimamia kuondoa wamachinga na kuweka jiji safi, lakini leo mambo yamebadilika.

Kwenye kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho kinachopokea magari kutoka ndani na nje ya jiji kama Chalinze, Kongowe na Mlandizi (mkoa wa Pwani), au Mkata (Tanga) na "Coster" za Morogoro wamachinga wametanda kila kona.

Juhudi za kuwapanga wafanyabiashara hao, zimeondoka na kituo hicho kinakabiliwa na changamoto nyingi ambazo ni kero kwa abiria zikiwamo zinazosababishwa na madereva wa daladala zinazofanya safari ndani na nje ya jiji.

Wanasiasa waliotumia nguvu na mikakati ya kupunguza wamachinga hao leo wanashuhudia kituo kilivyojaa vibanda na pia magari yakiegeshwa ovyo na kufanya vile wanavyopenda.

Kwa mfano magari ya mkoa wa Pwani kama ya Mlandizi, Kongowe na Vigwaza hutoka kituoni yakiwa tupu na kusimama katikati ya barabara ndani na nje ya kituo kuita abiria na kuongeza foleni pia kuziba sehemu za kupita.

Wakati madereva wakifanya mchezo huo, baadhi ya wenzao wa daladala husimama sehemu ya wazi inayotumiwa daladala zilizojaza abiria na kuanza kusaka abiria.

Katika mazingira hayo, daladala zenye abiria zinashindwa kupita, mabasi ya mwendo wa haraka nayo yanakwama, hivyo wakati mwingine zinaweza kupita dakika 20, abiria wakiwa 'wameganda' kituoni hapo.

Hali kama hiyo imekuwa ni ya kawaida kituoni hapo kana kwamba ni haki yao kufanya usumbufu huo ambao husababisha usumbufu usio wa lazima kwa abiria wanaowahi kazini au katika shughuli zao za kila siku.

Mkuu wa Trafiki Wilaya ya Kimara (DTO), Hadija Said, anakiri kuwapo kwa tatizo hilo miezi ya nyuma, na kwamba alishalifanyia kazi siku nyingi na kusema anashangaa kusikia bado lipo.

Anaahidi kulifuatilia ajue kuna nini, kwani wapo askari wanaohudumia kituo hicho.

Kamanda huyo anaongeza kusema; "Nimewaweka meja mmoja na mkaguzi mmoja, nataka niwaulize shida ni nini, mmpewa eneo, hapo kuna shida gani watu wanaleta malalamiko."

Anasema, hawezi kujigawa na kufika kila sehemu kwa wakati mmoja, na kwamba ndiyo maana ameweka askari eneo ili kitu kiende sawa, na kwamba anashangaa kusikia malalamiko yakiendelea kuwapo.

"Tulishapata malalamiko na kuyashughulikia, ni zaidi ya mwezi sasa, lakini ninashangaa kusikia kwamba bado yapo, kama abiria wataona foleni ya aina hiyo huku askari akiwapo bila kuchukua hatua, ni vyema wakanakiri namba yake ya kazi wanitumie," anasema.

Meneja wa Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Dar es Salaam, John Mkumbo, anasema amepokea malalamiko na kwamba atayafanyia kazi ili kumaliza kero hiyo kwa abiria.

Anafafanua kuwa awatawasiliana na wadau wengine, hasa polisi kupata taarifa zaidi kuhusu changamoto hiyo, na kupanga jinsi ya kuishughulikia kwa pamoja, ili kuwaondolea abiria usumbufu.

"Lakini sio vibaya nikapata ushauri wako, wewe una ushauri gani kwenye jambo hilo kama mmoja wa abiria wanaotumia kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho," anasema Mkumbo.

**USHURU KITUONI**

Kuhusu vijana wanaokusanya ushuru kituoni, wakizuia daladala kupita kwa kuweka mbele vyuma vyenye misumari na mapipa, Mkumbo anasema kwa kifupi bila kufafanua kuwa TANROADS haina utaratibu wa kukusanya pesa kwa mtindo huo.

Mjumbe wa Bodi ya Taasisi ya Kutetea Haki za Abiria (TAKUHA), Hassan Mchanjama, anasema, TANROADS Mkoa wa Dar es Salaam na trafiki wilaya ya kipolisi Kimara, hawana budi kumaliza kero hiyo, kwa kuwa ndio wadau wakuu wa usafiri kituo hicho cha daladala.

"Ni kwamba, mmoja anasimamia kituo na mwingine anasimamia sheria, hivyo ni vyema wakaweka mikakati ambayo itasaidia kumaliza tatizo hilo la muda mrefu," anasema Mchanjama.

Anasema, TAKUHA inatambua juhudi zinazofanywa na wadau hao, na kuongeza kuwa tatizo lililopo ni baadhi ya madereva na makondakta kutofuata sheria hadi washurutishwe.

"Kwa kuwa ndivyo wanavyotaka, basi niwaombe polisi wafanye hivyo, ili kumaliza kero hiii kwa abiria wetu, kwani taaisisi yetu ina taarifa za usumbufu unaosababishwa na baadhi ya madereva hao," anasema.

Mchanjama anasema, kitendo cha dereva kutoa daladala kituoni na kwenda kusimamisha barabarani kusubiri abiria si cha kuvumilia, kwa kuwa kinaleta usumbufu mkubwa kwa wengine.

"Fikiria kuwa daladala imeshajaza abiria lakini haitoki kituoni eti kwa sababu kuna dereva mwingine ameziba barabara kusubiri abiria, kwa nini asijaze akiwa kituoni kisha aondoke? Hii ni kero," anasema Mchanjama.

## JOPO LA WANASHERIA WA KAMPENI YA SAMIA WALIVYOMTOA GEREZANI ALIYEBAMBIKWA KESI

**INATOKA UK. 11**

indi fulani inamalizika ikifanywe kiwe kitu cha kudumu au taasisi ya kudumu kama ilivyo ya Benjamini Mkapa ili iendelee kusaidia wanyonge wanaokosa haki."

Ester Lihofo, anasema kampeni hiyo ni msaada mkubwa kwa wananchi na kwamba ni vema ikafika katika maeneo mengi ili Watanzania wengi wenye shida ya kutafuta haki wasaidiwe.

"Wengi wanakosa au kudhulumiwa haki zao lakini wanaamua kukaa kimya kwa sababu hawana uwezo kulipia gharama za wanasheria mahakamani, lakini hapa ukifika unasaidiwa bure, huu ni msaada mkubwa tutashukuru sana," anasema Easter.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Eliakimu Maswi, akizungumzia mafanikio ya Kampeni Msaada wa Huduma za Kisheria ya Mama Samia, akiwa kwenye Banda la Katiba na Sheria, katika Maonesho ya Kilimo Kitaifa Nanenane, jijini Dodoma, anasema Msaada wa Huduma za Kisheria ya Mama Samia, imehudumia wengi kwenye migogoro ya mirathi na ardhi.

Anasema katika mirathi wanaofika kwa msaada wa huduma za kisheria ni wanawake.

# Ndivyo tume inavyoshirikisha wadau uchaguzi katika kuboresha daftari

**Na Bartholomew Wandi, INEC**




Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji Jacobs Mwambegele, akizungumza katika mkutano wa wadau wa uchaguzi kuhusu kuboresha daftari la kudumu la wapigakura. **PICHA: INEC**

OKTOBA mwaka huu ni uchaguzi wa serikali za mitaa, unaohusisha kuchagua wenyeviti na wajumbe wa kuviongoza vijiji, vitongoji na mitaa na baadaye utafuata uchaguzi mkuu kupata rais, wabunge, masheha na madiwani 2025.

Ni katika kipindi cha kuelekea kwenye uchaguzi mkuu 2025, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) inawashirikisha wadau wa uchaguzi kuanza mchakato wa kuboresha daftari la wapigakura kwa njia mbalimbali.

Mathalani kwa njia ya mikutano na wadau wa uchaguzi kwenye mikutano ya kitaifa iliyofanyika Dar es Salaam kuanzia Juni 7 hadi 15, 2024 ikiwashirikisha viongozi wa vyama vya siasa, wa dini na asasi za kiraia.

Pia, INEC kupitia mikutano hiyo inayafikia makundi mbalimbali ambayo ni vijana, wanawake, wenye ulemavu, wazee wa kimila, uhamiaji, polisi, wahariri, waandishi wa vyombo vya habari na maofisa habari wa mikoa na halmashauri.

Mikutano hiyo pamoja na wadau wa uchaguzi kwa ajili ya kupeana taarifa ya kuanza kuboresha daftari la kudumu la wapigakura ilianza kwa kukutana na viongozi wa vyama vya siasa.

Akizungumza na wajumbe hao, Mwenyekiti wa Tume, Jaji (Rufani), Jacobs Mwambegele, anawaambia viongozi hao kuwa wataruhusiwa kuweka wakala mmoja kwenye kila kituo cha kuandikisha wapigakura.

Anawaeleza kuwa lengo la kushuhudia utekelezaji wa kazi ya kuboresha daftari hilo vituoni ni kufanikisha kuwatambua wale wanaokuja kituoni kama wana sifa za kuandikishwa kwenye daftari la kudumu la wapigakura

INEC inapokutana na viongozi wengine mbalimbali kuanzia wa dini, asasi za kiraia, wanahabari na makundi ya wanawake, vijana na wenye mahitaji maalumu, lengo ni kuwapa taarifa ya zoezi la kuboresha daftari ambao ulizinduliwa mkoani Kigoma, Julai 20 mwaka huu.

Aidha wanafahamishwa kuwa kazi ya kuliboresha itafanyika siku saba kwa kila kituo na vituo vitafunguliwa kuanzia saa 2:00 asubuhi na kufungwa saa 12 jioni.

Dhumuni lingine ni kuwashirikisha wadau hao wa uchaguzi kutoa taarifa sahihi kwa wananchi wote walio na sifa za kuandikishwa waende wakaandikishwe na wanaotaka kuboresha taarifa, wakaziboreshe na ambao kadi za mpigakura zimepotea au kuharibika waende vituoni wakapate mpya.

Zaidi ya hayo, tume pia inatoa fursa ya kukutana na wadau wa uchaguzi katika mikoa mitatu ambayo itaanza zoezi la kuboresha daftari la kudumu la wapigakura Julai 20, 2024.

Mkoani Kigoma INEC ilikutana na wadau wote wa uchaguzi kwa pamoja mkoani Kigoma Juni 19, 2024 na kisha ikakutana na wadau wengine wa uchaguzi wa mikoa ya Katavi na Tabora Julai 08, 2024.

Madhumuni ya mikutano ni pamoja na kusisitiza zaidi kazi ya kuboresha huko mikoani ambako wananchi wapo na watafuatwa hadi kwenye vitongoji ambako vituo vya kupigia kura pia vipo huko.

Zoezi la kukutana na wadau mikoani litaendelea kulingana na ratiba iliyopangwa na tume ambapo mikoa ya Geita na Kagera kikao kitafanyika Julai 24, na uboreshaji wa daftari utaanza Agosti 05 hadi 11, Mwanza na Shinyanga utafanyika Agosti 09, uboreshaji utaanza Agosti 21 hadi 27.

Mikoa ya Mara, Simiyu na Manyara katika Halmashauri za Wilaya ya Babati, Hanang, Mbulu na Mji wa Babati utafanyika Agosti 25, wakati uboreshaji wa daftari utafanyika kuanzia Septemba 04 hadi 10 mwaka huu.

Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara katika Halmashauri za Wilaya za Kiteto, Simanjiro na Mji wa Mbulu utafanyika Septemba 13 na uboreshaji utafanyika kuanzia Septemba 25 hadi Oktoba 1, 2024.

Kwa Zanzibar ni Oktoba 03 na kufuatiwa na uboreshaji utakaofanyika Oktoba 11 hadi 17. Aidha, kwa mikoa ya Singida na Dodoma katika halmashauri za wilaya ya Chamwino, Kongwa, Chemba, Bahi, Kondoa, Kondoa Mji wa na Dodoma Jiji mkutano wa wadau utafanyika Novemba 29, 2024. Utafuatiwa na uboreshaji utakaofanyika Desemba 11 hadi 17.

Mikoa ya Iringa, Mbeya na Dodoma katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa mkutano wa wadau utafanyika Desemba 15, na uboreshaji utafuata Desemba 27 , 2024 hadi Januari 2, 2025.

Mikoa ya Njombe, Rukwa, Songwe na Ruvuma katika halmashauri za wilaya za Nyasa, Mbinga, Mji ya Mbinga, Wilaya ya Songea na Manispaa ya Songea mkutano wa wadau utafanyika Desemba 31, 2024 na uboreshaji wa daftari utafanyika Januari 12 hadi 18, 2025.

Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma katika halmashauri za wilaya za Madaba, Namtumbo na Tunduru, mkutano wa wadau utafanyika Januari 16, 2025 na uboreshaji utafanyika Januari 28, 2025 hadi Februari 3.

Kwa mikoa ya Pwani na Tanga katika Halmashauri za Wilaya ya Lushoto, Kilindi, Muheza, Korogwe, Korogwe Mji Handeni Mji na Tanga Jiji utafanyika tarehe 01 Februari, 2025 na uboreshaji utafanyika Februari 13 hadi 19, 2025.

> Zoezi la kukutana na wadau mikoani litaendelea kulingana na ratiba iliyopangwa na tume ambapo mikoa ya Geita na Kagera kikao kitafanyika Julai 24, na uboreshaji wa daftari utaanza Agosti 05 hadi 11, Mwanza na Shinyanga utafanyika Agosti 09, uboreshaji utaanza Agosti 21 hadi 27.

Pamoja na hayo, Morogoro na Tanga katika Halmashauri za Wilaya ya Bumbuli, Handeni, Pangani na Mkinga utafanyika Februari 17, 2025 na uboreshaji wa daftari utafanyika Machi 1 hadi 7, 2025.

Kwa Dar es Salaam mkutano wa wadau ni Machi 5, 2024 na uboreshaji wa daftari utafanyika Machi 17 hadi 23, 2025.

Aidha, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imeanzisha Kituo cha Huduma kwa Wateja (Call Centre) ambacho kitawahudumia wote wanaotaka kufahamu masuala ya kuboresha daftari kwa kuongea na ofisa wa tume moja kwa moja.

Wananchi hao wataongea moja kwa moja na ofisa wa tume kwa kupiga namba 0800112100 bure kwa kutumia simu zao za kiganjani.

Itakumbukwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ni taasisi huru iliyoanzishwa kwa mujibu wa ibara ya 74(1) ya Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977.

Tangu kuanzishwa Januari 13, 1993, imesimamia uchaguzi mkuu sita wa mwaka, 1995, 2000, 2005, 2010, 2015, 2020. Uchaguzi unaokuja mwaka 2025 utakuwa wa saba.

Kujiandikisha kuwa mpigakura ni msingi wa uchaguzi bora

Mwenyekiti wa JUWAUZA , Salima Haji Sadat.

JUKWAA LA VIONGOZI

# SAMBI KATIKA MIKONO YA WASIOMTAKIA MEMA

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa zamani wa Comoro, Sayyid Ahmed Sambi (66), kwa sasa anatumikia kifungo cha maisha jela, kutokana na kile serikali inachodai kuwa ni hatia ya uhujumu uchumi na uhaini.

Ni mambo yanayofanywa na serikali ya Rais Azali Assoumani, anayeongoza visiwa hivyo kwa sasa.

Lakini wakati Sambi akiwa jela, kutokana na kesi hiyo, wengi wanaona kama ni kuzima harakati zake za siasa na kile kinachoonekana kuwa Rais Assoumani anamwogopa.

Sambi, aliyezaliwa Juni 5, 1958 ni maarufu zaidi kwa jina la 'Ayatollah', akiingia madarakani baada ya kushinda uchaguzi wa Mei 14, 2006 kwa kupata asilimia 58.2 ya kura zote.

Ilipofika Mei 26, 2006, Sambi aliapa kuwa Rais wa Muungano wa Visiwa vya Comoro, akiwa kiongozi aliyeingia madarakani kwa kubadilishana uongozi kwa amani katika historia ya nchi hiyo.

Akiwa amezaliwa eneo la Mutsamudu, katika kisiwa cha Anjouan ni baba wa watoto saba na ni mfanyabiashara maarufu na alianzisha pia kituo chake cha runinga kiitwacho Ulezi.

Rais mstaafu huyu ni mbobezi katika elimu ya Dini ya Kiislamu, akisoma nchini Sudan, Saudi Arabia na Iran na alikokuwa chini ya usimamizi wa Ayatollah Mesbah Yazdi na ndiko alikojipatia jina maarufu mpaka sasa la Ayatollah wa Comoro.

KUSHTAKIWA

Mahakama ya Comoro ilimhukumu Sambi kifungo cha maisha, baada ya kumtia hatiani kwa makosa ya uhaini yanayohusishwa na kuuza hati za kusafiria za nchi hiyo kwa raia wa kigeni.

Sambi, ni hasimu mkubwa wa Rais Assoumani, amehukumiwa na Mahakama Maalum ya Usalama wa Taifa, chombo maalum ambacho hukumu zake haziwezi kukatiwa rufani.

Rais wa mahakama hiyo, Omar Ben Ali, anasema wakati wa kusoma hukumu: "Sambi anahukumiwa kifungo cha maisha. Mahakama hii inaamuru mali zake zote kutaifishwa kwa maslahi ya umma."

Mstaafu huyo anapewa adhabu hiyo wakati mwenyewe akiwa hayupo mahakamani baada ya kukataa kuhudhuria vikao vya kesi hiyo.

Amewahi kushiriki kwa muda mfupi wakati kesi ilipotajwa kwa mara ya kwanza, mawakili wake wakamwomba jaji kujitoa kwani aliwahi kuwa sehemu ya jopo la waendesha mashtaka. Ombi hilo likatupwa.

Sambi anasema kuundwa kwa mahakama yenyewe ni kinyume cha sheria na asingependa kuhukumiwa na mahakama ya aina hiyo.

Binti wa Sambi, Tisslame Sambi, anasema hukumu yenyewe ilenga kile ambacho wamekuwa wakikisema tangu awali.



Mfungwa wa kisiasa Rais Mstaafu, Sayyid Abdallah Sambi. **PICHA: MTANDAO**

"Jopo la dhihaka kwenye mahakama inayoongozwa na wajumbe wa serikali ambayo inatoa hukumu ya kifungo cha maisha kwa mpinzani mkubwa wa utawala uliopo madarakani."

Sambi, aliyeliongoza taifa hilo dogo ndani ya Bahari ya Hindi, mwaka 2006 na 2011, alipitisha sheria inayoruhusu uuzaji wa hati za kusafiria kwa bei ya juu, kupitia mpango ulioitwa 'bidoon', neno la Kiarabu linalomaanisha maelfu ya watu ambao hawawezi kupata haki ya uraia.

Jean-Gilles Halimi ni mmoja wanaomuunga mkono Sambi , anasema hakuna ushahidi wowote wa fedha zilizopotea ama akaunti za benki ambazo ziliwasilishwa mahakamani kuonesha jinsi ufisadi ulivyofanyika.

**HARAKATI ZA KUMFUNGA**

Wachambuzi wanasema, walimwandalia mashtaka na kesi yake ikapelekwa katika mahakama maalum ambayo hukumu zake hazipingwi.

Wakati anatua Comoro, huku akipokelewa na maelfu ya wafuasi wake uwanja wa ndege, alipinga vikali kura ya maoni ya marekebisho ya katiba, iliyokuwa inapendekezwa na serikali ya Assoumani. Hayo yalitokea mwaka 2018.

Ni katika hotuba yake ambapo alitamka msemo ambao umekuwa maarufu kama ibada kwa Wacomoro wengi wa 'siogopi haki, naogopa dhuluma.'

Siku saba baada ya kuwasili Mei 19, 2018, aliwekwa chini ya kizuizi cha nyumbani kwa amri ya moja kwa moja ya Rais Assoumani.

Tangu siku hiyo, Sambi hajawahi kupata tena uhuru wake na miezi mitatu baadaye, Rais Assoumani alikiri katika mahojiano ya kushtua aliyofanya na gazeti la AfriquEducation Agosti 2018.

Kwa mujibu wa Katiba ya Comoro, mahakama pekee ndiyo yenye mamlaka ya kumnyima raia uhuru wake, kwa kumfunga na si kumweka kizuizini.

Baada ya kibano cha muda mrefu, Sambi aliondolewa katika kifungo hicho cha nyumbani Agosti 19, 2018, hakujulishwa kuhusu kesi hadi Oktoba, hivyo akaendelea kuwapo kizuizini kumbe alikuwa huru kwa miezi miwili iliyopita.

Wakati Agosti 19, 2018 ilikuwa ndiyo siku yake ya mwisho kuwekwa kizuizini, akiwa hajapewa taarifa yoyote ya kuwa huru, siku inayofuata Agosti 20, mwaka huo Sambi alifuatwa na kuelezwa kwamba anawekwa kizuizini, kabla ya kuanza kwa kesi inayomsubiri.

Anayeeleza hayo mbele ya Sambi alikuwa ni Jaji Mchunguzi wa Mahakama ya Moroni, Aliamane Ali Abdallah, huku akimsomea vifungu kadhaa vya Kanuni ya Adhabu na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Comoro.

Safari hii, hati hii ya kuwekwa kizuizini inahusu mashtaka kadhaa kwa makosa yanayodaiwa kutendwa alipokuwa mkuu wa nchi, jambo la kushangaza ni kwamba anatuhumiwa kwa vitendo ambavyo inadaiwa alivifanya mwaka 2017, akiwa si rais tena wa Muungano wa Comoro, kwani kushika kwake madaraka kulikoma Mei 26, 2011.

"Kuwekwa kizuizini hakuwezi kuzidi miezi minne. Hata hivyo, baada ya muda huu kuisha, mwendesha mashtaka anaweza kuongeza muda huo kwa kutoa amri kama inavyoelezwa na sheria."

Hii ina maana kwamba hakuna muda utakaoongezwa mara baada ya miezi minne kumalizika, lakini ijulikane kwamba Sambi aliwekwa kizuizini kabla ya kusikilizwa kwa kesi kuanzia Agosti 20, 2018 hadi kesi yake aliyobambikiwa ilipoanza Novemba 2022, yaani zaidi ya miaka minne akiwa kizuizini.

**KUKATALIWA MATIBABU**

Wakati akiendelea kushikiliwa, Sambi ananyimwa fursa ya kukutana na madaktari kutokana na matatizo ya kiafya aliyokuwa nayo, hasa ya meno.

Imetokea mara kadhaa kwamba ombi rahisi la mashauriano ya matibabu kwa daktari wa meno, lilichukua karibu siku 10 kabla ya kukubaliwa, kwa sababu licha ya idhini iliyotolewa ya kumpa fursa ya kukutana na daktari, mwendesha mashtaka aliweka pingamizi ili kuchelewesha.

Sambi amechunguzwa mara mbili na madaktari wawili waliotumwa na serikali.

Familia yake inaomba mahakama iidhinishe kwa mtu wao kwenda kupatiwa matibabu nje ya nchi, Jaji Aliamane Ali Abdallah aliidhinisha hilo kwa kuachiliwa kwa muda, Januari 2, 2020 kama ilivyopendekezwa na daktari wake.

Serikali ya Comoro ilizuia kumpa ruhusa ya kwenda kutibiwa nje, kwani kila kitu kilikuwa tayari kimepangwa.

**MFUNGWA WA KISIASA**

Kutokana na Serikali ya Comoro kutotii amri ya mahakama, Sambi amekuwa mfungwa wa kisiasa na kuachiliwa kwake ni lazima jamii ya kimataifa ipaze sauti.





# Waandishi, mawakili wapigwa msasa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISI ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) kupitia Ofisi ya uandishi wa sheria imeendesha mafunzo kwa waandishi wa sheria na mawakili wa serikali kwa ajili ya masuala ya kuzingatia wakati wa kuandaa na kurekebisha sheria ndogo na kanuni.

Mwandishi Mkuu wa Sheria, Onorius Njole, akizungumza wakati wa mafunzo hayo jijini hapa juzi, alisema ni mahususi kwa waandishi wa sheria na mawakili kuwajengea uwezo wa kutatua changamoto zinazoibuliwa na Kamati ya Bunge ya Sheria ndogo na kuongeza ufanisi wakati wa uandaaji na uandishi wa sheria ndogo na kanuni.

"Mafunzo ya leo ni maalumu katika kupitishana kwenye hizo changamoto zinazoibuliwa na Kamati ya Kudumu ya Sheria ndogo ya Bunge, pia ni sehemu ya kujifunza ili tusiendelee kurudia tena hizo changamoto, hivyo yalikuwa mafunzo muhimu sana kwa waandishi wa sheria,"alisema

Alisema hivi karibuni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imetoa mwongozo kuhusu utaratibu wa uwasilishaji wa marekebisho ya sheria, kanuni na utengenezaji wa kanuni mpya.

"Na mwongozo mwingine ni kuhusiana na utaratibu wa kushughulikia hoja zinazoibuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria ndogo,"alisema

Alisema lengo la kutoa miongozo hiyo ni kupunguza changamoto ambazo zimekuwa zikijitokeza kwenye sheria na kanuni ambazo zinakuja kufanyiwa marekebisho.

Alisema malalamiko kwenye baadhi ya kanuni kutokidhi malengo yaliyokusudiwa kumesababisha ofisi hiyo kutoa maelekezo mahususi katika kutatua changamoto hiyo.

"Baadhi ya kanuni zimekuwa zikilalamikiwa kutokidhi malengo yaliyokusudiwa kwa sababu ya kutokuwa na maelekezo toshelevu kutoka kwenye wizara husika, hali hiyo imepelekea Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutoa maelekezo ya kutunga sheria na kanuni au sheria ambayo itakidhi yaliyokusudiwa," alisema

Akiwasilisha mada wakati wa mafunzo hayo, Mwandishi Mkuu wa Sheria Msaidizi, Nicodemus Chuwa, alisema mada kuu zilikuwa ni majukumu ya mwandishi wa sheria wakati wa kuandaa sheria ndogo.

Wakili wa Serikali, Stephano Mbutu kwa niaba ya washiriki, alipongeza Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa kuandaa mafunzo hayo kwa kuwa yanawasaidia kuongeza ujuzi na ufanisi kwenye kazi zao.

# Baraza la Taifa la Vijana mbioni kuanzishwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imezindua sera mpya ya taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 toleo la 2024 kwa ajili ya kutatua changamoto za vijana na kutoa mwongozo wa kuanzishwa rasmi kwa Baraza la Taifa la Vijana.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi,Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete alibainisha hayo jana jijini hapa wakati akihutubia kwenye maadhimisho ya Siku ya Vijana Kimataifa.

"Serikali imekwisha kamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Vijana ya mwaka 2007 na marekebisho yake yamefanyika mwaka 2024 na leo hii tunakwenda kuizindua muda mfupi ujao.

"Ndugu washiriki changamoto nyingi zinazoelezwa kwa vijana zinatokana na ukweli kwamba yapo baadhi ya maeneo hayana miongozo yake kupitia sera hii ya vijana ambayo tutaizindua leo nina hakika kabisa vilio vya vijana wengi vinakwenda kupatiwa ufumbuzi baada ya kupitishwa kwa sera hii," alisisitiza Ridhwani.

Alitoa wito kwa maofisa kazi kutambua kuwa nafasi zao siyo za kukaa ofisini wakisubiri vijana kwenda kulia na kueleza changamoto zao.

Alisema nafasi za maofisa hao wa wizara hiyo ni kwenda kukutana na vijana katika maeneo mbalimbali nchini na kutambua changamoto zao na kuzipatia majibu.

"Ndugu washiriki katika nukta hii naomba nieleze baadhi ya mambo ambayo yanakwenda kufanyiwa marekebisho na sera yetu hii 2007 toleo la 2024 ambayo tunakwenda kuizindua leo," alisema Ridhiwani na kuongeza kuwa:

"Sera hii ifahamike ni matokeo ya vilio vya vijana walio wengi ambavyo vilisikika kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ambaye wakati anahutubia vijana mkoani Mwanza Juni 15, mwaka 2021 aliielekeza wizara yetu kuangalia changamoto za vijana na kuzitafutia majawabu leo hii nimesimama mbele yenu ninayofuraha kubwa kuwaeleza vilio vyenu vimepatiwa njia ya kwenda kuvikabili."

Alisema sera hiyo inaeleza uelekeo na njia ambazo wanakwenda kuzitumia ili kufikia malengo ambayo yata tatua matatizo waliyonayo vijana.

"Sera hii inakwenda kuanzisha Baraza la Taifa la Vijana na kuwa mwarobaini wa kutambua na kutatua changamoto nyingi za vijana.

"Vijana wamekosa maeneo ya kueleza changamoto zao, walikosa watu wa kuwasikiliza, msukumo wa kufikisha changamoto zao na kuzitafutia majawabu kwa pamoja"alisema

Alisema, ujio wa sera hiyo na uundwaji wa baraza hilo unaonesha azma ya Rais Samia kujidhatiti na changamoto zinazowakabili vijana ili zipatiwe majibu.

Pia, Ridhiwani alisema sera hiyo inakwenda kutambua vijana katika sekta zote wanaofanya kazi katika maeneo hatarishi ikiwamo sekta ya madini, uzalishaji mali ikiwamo mashambani na kwenye mifugo.

"Wapo vijana wanaofanya kazi za sanaa ikiwamo ubunifu, muziki, michezo, utungaji wa kazi za kisanaa. Sera hii inakwenda kugusa katika maeneo hayo.




Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, SACP Anania Amo, akizungumza na waandishi wa habari, jijini humo jana, wakati akitoa taarifa ya hali ya ulinzi na usalama kwa mkoa huo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Kinachokwamisha wanafunzi kufikia malengo

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

OFISA Elimu wa Mkoa wa Singida, Dk. Elipidius Baganda amesema changamoto ya mdondoko wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari inakwamisha kufikia malengo ya elimu.

Dk. Baganda alisema hayo juzi wakati wa mafunzo maalum ya Mpango wa Shule Salama kwa washiriki 275 kutoka mikoa ya Singida, Shinyanga, Tabora na Simiyu yaliyoandaliwa na Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Alisema serikali imeanzisha mpango huo katika shule za sekondari nchini kwa lengo la kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji ili kuongeza ulinzi na usalama wa watoto.

Dk. Baganda, alisema serikali imechukua hatua za kupambana na changamoto hiyo ikiwa ni pamoja na kutoa elimu bila malipo na kujenga shule za sekondari karibu na makazi ya wananchi ili kupunguza umbali wa kufuata shule.

"Serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, inaendelea kutambua na kuthamini elimu kama chombo muhimu cha kuleta maendeleo, hivyo kuna haja ya kusisitiza umuhimu wa elimu bora kwa wanafunzi kama msingi wa maendeleo ya taifa," alisema.

Dk. Baganda, aliwashukuru wadau wanaoshiriki kusimamia utekelezaji wa mpango huo na kuwataka kujadiliana, kubadilishana uzoefu na kutumia mafunzo hayo kuibua mbinu mpya za kuboresha mazingira ya shule na kuhakikisha wanafunzi wanakamilisha mzunguko wa elimu kwa mafanikio.

Mafunzo hayo ya siku tatu yanafanyika mkoani Singida kuwajengea uwezo washiriki na kuhakikisha shule za sekondari zinatoa elimu bora kwa kuondoa vikwazo kwa wanafunzi.

Mafunzo hayo yamehusisha wenyeviti wa bodi za shule za sekondari 150, maofisa 12 , maofisa maendeleo ya jamii mkoa na waratibu wa mpango huo.

Waratibu wa programu ya SEQUIP nao walishiriki katika mafunzo hayo ambayo ni sehemu ya mpango wa kuboresha elimu ya sekondari kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2020 hadi 2025.

Lengo kuu la mafunzo hayo ni kuwapatia stadi na mbinu za usimamizi bora wa shule za sekondari ili kuhakikisha elimu inayotolewa inakidhi viwango.

Pia, mafunzo hayo yanazingatia kuondoa vikwazo kama vile ukosefu wa chakula, utoro na matumizi ya viboko, ambavyo mara nyingi huzuia wanafunzi kufikia malengo yao ya ufaulu mzuri.



# Mfanyakazi baa auawa madai kusababisha hasara ya 50,000/-

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe linamshikilia Michael Gwivaha (33) kwa tuhuma za mauaji ya aliyekuwa mfanyakazi wake wa baa, Faraja Mbembela kwa kudaiwa kusababisha hasara ya Sh. 50,000 na mwili wake kutupwa katika misitu ya Tanwat uliopo mkoani hapa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi Mahamoud Banga alieleza hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana.

Alisema tukio hilo lilitokea Julai 14 mwaka huu majira ya saa 10 alfajiri katika Kijiji cha Lusisi, wilayani Wanging'ombe, huku chanzo kikitajwa kuwa katika mahesabu wakati wa kukabidhiana kati ya Faraja na bosi wake, kulionekana kuna hasara ya Sh. 50,000.

Kamanda Banga alisema Faraja aliuawa kwa kushambuliwa sehemu mbalimbali za mwili kwa kupigwa ngumi akiwa ndani ya baa na baadaye kumwagiwa mafuta ya petroli na kuchomwa moto kwenye mapaja.

"Mtuhumiwa baadaye alibeba mwili wa marehemu katika mfuko wa sandarusi na kwenda kuutupa misitu ya Tanwat ili asigundulike," alisema Kamanda Banga.

Alisema kuwa, taratibu za kumfikisha mahakamani mtuhumiwa huyo zinaendelea ili kwenda kujibu tuhuma zinazomkabili.

Katika tukio lingine, Kamanda Banga alisema Jeshi la Polisi, linamshikilia Nicholaus Mtega, mkazi wa Kambarage, mjini Njombe kwa tuhuma za mauaji ya dereva bodaboda.

Alisema Jeshi la Polisi pia linashikilia watuhumiwa saba wanaodaiwa kuhusika na mauaji ya kikongwe Tulivane Mtedzi (85) aliyeuawa katika Mtaa wa Idundilanga.

"Watu hawa tunaendelea kuwahoji, akiwamo mchunga ng'ombe aliyetoroka, naye tumemkamata na baadhi ya wana ndugu na wenyewe tutawafikisha mahakamani upelelezi utakapokamilika," alisema Kamanda Banga.

Alisema jeshi hilo pia linajivunia mafanikio kadhaa katika utendaji wake, ikiwamo kifungo cha miaka 30 gerezani alichohukumiwa Godfrey Magulu baada ya kupatikana na hatia ya kubaka wilayani Wanging'ombe, mkoani Njombe.

Alisema Yona Kidenya amehukumiwa kifungo cha maisha gerezani kwa kosa la kubaka katika wilaya hiyo, huku Gudluck Mgaya akifungwa miaka mitano kwa kosa la unyang'anyi wa kutumia nguvu huko Mundindi, wilayani Ludewa.

Kwa upande wa usalama barabarani, alisema Jeshi la Polisi likamata makosa 4,912, kati yake, mmoja alifikishwa mahakamani na wawili kufungiwa leseni, huku waliolipa faini wakiwa 4,909.

Alisema jeshi hilo linaendelea kutoa wito na kuwakumbusha madereva kutii sheria za usalama barabarani na kuacha kujichukulia sheria mkononi.



Sehemu ya umati wa madereva wa bajaji wa Jiji la Mbeya, wakimsikiliza Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa (NEC) Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela (hayupo pichani) alipokuwa akisikiliza kero zao, jijini humo juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# CCM yawataka madereva bajaji kuwasilisha kero

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, kimewataka viongozi wa madereva bajaji wa wilaya zote za mkoa huo kukutana na kuainisha kero zinazowakumba, ambazo zinafanana katika maeneo yote na kuziwasilisha kwenye ofisi za chama hicho ili zitafutiwe ufumbuzi.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), Ndele Mwaselela anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, aliyasema hayo juzi alipofanya kikao na madereva bajaji wa Jiji la Mbeya kwa lengo la kusikiliza kero zinazowakabili.

Alisema baada ya kero hizo kuwasilishwa, viongozi wa chama hicho watashirikiana na viongozi wa serikali pamoja na watendaji wa halmashauri zote kuzijadili na kuzitatua kwa pamoja ili vijana ambao wameajiriwa kwenye kazi hiyo wafanye kazi kwa uhuru.

Alisema bajaji ni miongoni mwa vyombo vya usafiri ambavyo vimeajiri kundi kubwa la vijana na hivyo akasisitiza kwamba ni lazima kero zinazowakabili zitatuliwe mapema.

"Kuna baadhi ya kero zinawakumba madereva bajaji kwenye halmashauri zote katika mkoa wetu, sasa ni vigumu sisi kama viongozi kuzijua, ndiyo maana tunataka viongozi wenu watuainishie kero hizo ili tukae na kujadili namna ya kuzitatua," alisema Mwaselela.

Alisema madereva hao wanapokumbwa na matatizo wanatakiwa kuwapatia taarifa viongozi wao ili wao ndiyo waziwasilishe kwenye ofisi za chama kwa ajili ya kuzishughulikia.

Hata hivyo aliwataka madereva wa bajaji kufanya kazi kwa kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kulinda maisha yao pamoja na maisha ya wateja wanaokuwa wamewabeba.

Mwenyekiti wa Chama cha Madereva Bajaji Jiji la Mbeya, Lucas Mwakyusa alisema madereva bajaji wamekuwa wakikabiliwa na matatizo mbalimbali ambayo yanasababisha kazi yao kuwa ngumu na hivyo kutowapatia faida wanayostahili.

Alisema moja kati ya kero zinazowakabili ni pamoja na ubovu wa barabara wanazozitumia ikiwemo ya Mwanjelwa- Mapelele ambayo alisema ni mbovu na hivyo inasababisha uharibifu wa vyombo vyao.

Vilevile alisema kutokana na barabara hizo kuwa za vumbi wamekuwa wakichafuka wao pamoja na abiria wao na hivyo akawaomba viongozi wa CCM kuwasaidia kutatua kero hiyo.

"Lakini tumekuwa tukiumizwa na maofisa wa TARURA ambao wamekuwa wakitukamata na na kututoza faini kubwa kwa makosa madogo madogo yakiwemo ya maegesho, wamekuwa wakitutoza mpaka sh. 50,000," alisema Mwakyusa.

Alisema kero nyingine ambayo inawakabili ni pamoja na kuzuiwa kuingia na bajaji ndani ya vituo vikubwa vya mabasi vya mkoa huo ikiwemo Kituo Kikuu cha Mabasi na Kituo cha Nane nane.

Kwa Upande wake Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa alisema atafuatilia baadhi ya kero zinazolalamikiwa na waendesha bajaji hao hasa zinazosababishwa na maofisa wa serikali ili azishughulikie mapema na kukipunguzia mzigo chama cha mapinduzi.

Moja ya kero alizosema atazishughulikia ni pamoja na zinazosababishwa na maofisa wa TARURA kuwakamata madereva hao pamoja na kuwapatia namba za malipo ambazo zinakuwa hazikubali kulipia.

## TARI yaanza utafiti wa majaribio mbegu za soya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya imeanza kufanya utafiti wa majaribio ya aina 30 ya mbegu za soya ili kupata mbegu bora zitakazoongeza tija ya uzalishaji wa zao hilo.

Mtafiti Mbunifu wa Mbegu TARI, Michael Kilango alisema hayo wakati akitoa elimu kwa wakulima kuhusu namna ya kuongeza tija kwenye uzalishaji wa zao hlo ambalo alisema serikali imepata soko la uhakika nchini China.

Kilango alisema waliamua kufanya utafiti huo kutokana na mahitaji ya walaji katika soko la zao hilo ambao wanahitaji mbegu zenye protini nyingi pamoja na mafuta mengi.

"Mbegu tunazozifanyia utafiti zinatoka katika maeneo mbalimbali nchini na katika baadhi ya mataifa ya Afrika Mashariki, kati ya mbegu hizi 30 tunatarajia tupate aina tatu ambayo tutaipeleka katika Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI) ili isajiliwe," alisema Kilango.

Alisema msimu wa kwanza wa utafiti huo walipata aina nne za mbegu na kwamba baada ya kukamilisha utafiti wa sasa watafikisha mbegu saba ambazo watazisambaza kwa wakulima.

Alisema mbegu hizo zikitumika vizuri wakulima wanakuwa na uwezo wa kuvuna tani mbili hadi tatu kwa hekta moja na zina kiwango cha mafuta zaidi ya asilimia 25 pamoja na protini zaidi ya asilimia 40.

Alisema serikali bado inayo dhamira ya dhati ya kuinua zao la soya kwa kumsaidia mkulima kupata ruzuku ya pembejeo na masoko ya uhakika na hivyo wataalamu hao watazifanyia majaribio tena kwa msimu ujao ili kuharakisha utokaji wa mbegu hizo ili kutimiza malengo ya serikali.

Baadhi ya wakulima wa zao hilo walisema endapo utafiti wa mbegu hizo utafanikiwa wakulima wataongeza tija ya uzalishaji na kuongeza kipata chao tofauti na hapo awali lakini wakataka kutatuliwa kwa changamoto ya upatikanaji wa masoko.





## Mfumuko wa bei washuka kwa asilimia 0.39

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MTAKWIMU kutoka Kitengo cha Takwimu za Bei Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Hassan Jamal Hassan amesema mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Julai 2024 umepungua na kufikia asilimia 5.26 kutoka asilimia 5.65 katika kipindi cha Juni 2024.

Alitoa takwimu hizo juzi visiwani hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari Mazizini.

Alisema bidhaa zilizosababisha kupungua kwa mfumko wa bei kwa mwaka ni pamoja na mchele (4.4%), unga wa ngano (4.5%), unga wa sembe (8.8%), ndizi za mkono mmoja (7.5%) na ndizi za mtwike (18.6%).

Alisema kwa ujumla faharisi za bei zimeongezeka na kufikia 112.31 kwa mwezi Julai 2024 ikilinganishwa na 106.70 ambayo iliripotiwa kipindi cha Julai 2023.

Alisema kundi la bidhaa za chakula na vinywaji visivyo na kileo kwa kipindi cha Julai, limepungua na kufikia asilimia 8.96 ikilinganishwa na asilimia 10.33 iliyorikodiwa Juni 2024.

Alisema kwa upande wa mfumko wa bei wa Julai 2024, umepungua na kufikia asilimia 0.22 ikilinganishwa na asilimia 0.56 iliyorikodiwa katika Juni 2024.

Aidha, alisema mfumko wa bei wa bidhaa za chakula na vinywaji visivyo na kileo kwa Julai 2024, umepungua na kufikia asilimia 0.15 ikilinganishwa na asilimia 0.70 iliyorikodiwa Juni 2024.

Alizitaja bidhaa zilizosababisha kushuka kwa mfumko wa bei wa mwezi ni pamoja na mchele kutoka Mbeya (2.0%), mchele wa Jasmin (0.4%), samaki (1.6%), ndizi za mkono mmoja (5.2%), sukari nyekundu (1.1%) na petroli (1.5%).

Akizungumzia hali hiyo ya mfumko, Meneja Msaidizi - Uchumi kutoka Benki Kuu Tawi la Zanzibar, Shami Chamicha alisema kupungua kwa kasi ya mfumko wa bei ni hatua nzuri ya kiuchumi na malengo yaliyokuwepo ya kubakia kwenye tarakimu moja.

# Dk. Mwinyi: Wanachama CCM acheni siasa za chuki, ubaguzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, amewataka wanachama wa chama hicho kujiepusha na makundi ambayo yanajihusisha na siasa za chuki na ubaguzi ili kulinda amani ya nchi.

Alitoa wito huo jana Mkoa wa Kusini Unguja ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kutembelea kamati za siasa kuanzia ngazi ya matawi, wadi, jimbo hadi mkoa, hafla iliyofanyika katika ukumbi wa Dk. Shein Tunguu mkoani humo.

Alisema zipo nchi mbalimbali duniani ziliingia katika vita kutokana na maneno ya chuki na ubaguzi hali inayosababisha kuvunjika kwa amani katika nchi zao, hivyo aliwasisitiza wanachama kuacha kujihusisha na siasa za chuki.

Akizungumzia kuhusu ujenzi wa Barabara ya Tunguu Makunduchi, alisema serikali ipo katika mazungumzo na kampuni za ujenzi kwa ajili ya kujenga barabara hiyo na hivi karibuni ujenzi utaanza.

Pia, aliwaahidi wananchi wanaoishi katika Kisiwa cha Uzi Ng'ambwa kuwa serikali itahakikisha inaijenga barabara yao ili kuwawekea mazingira mazuri wananchi wa kijiji hicho na maeneo ya jirani.

Akizungumza kuhusu uwezeshaji wananchi kiuchumi alisema serikali imetenga Sh. bilioni 31.9 kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuwapa mikopo isiyo na riba wajasiriamali ili kujiajiri.

Akizungumzia kuhusu changamoto ya maji katika mkoa huo alisema serikali inajipanga kuja na mradi mkubwa wa maji kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, kwamba changamoto hiyo itamalizika.

Naye Katibu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Amina Salum Mnacho alisema wameandaa mkakati maalumu wa kuwaandikisha wanachama wenye sifa ya kupiga kura katika daftari la wapiga kura ili kutimiza haki yao ya kikatiba.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, alisema katika kipindi cha miaka mitatu wavuvi wa mkoa huo wamepatiwa boti 60 kwa vikundi 60 hali iliyosababisha wavuvi kuvua uvuvi wa kisasa na kuondokana na uvuvi haramu.

Alisema mbali na boti hizo, aliahidi kutoa boti 100 kwa ajili ya wavuvi wa Kusini ili kuondoa migogoro kwa wavuvi wakiwemo wa Chwaka na Marubi.

Ayoub akizungumzia kuhusu utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa upande wa barabara alisema kuwa ilani imeelekeza kujengwa kilo mita 68 za barabara katika Mkoa wa Kusini kwa kipindi cha miaka mitano.




Meneja Mkufunzi wa Benki ya Stanbic Tanzania upande wa wateja Maalum, Irene Bizere, akitoa mafunzo ya kuweka akiba kwa baadhi ya watoto na wateja maalum wa benki hiyo, jijini Dar ers Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Viongozi watakiwa kuwajengea imani wananchi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema ni muhimu kwa viongozi wa serikali na siasa kuhakikisha wanawajengea imani wananchi kuelekea Uchaguzi Mkuu mwakani ili kuepusha matatizo kujirudia.

Alitoa wito huo ofisini kwake Migombani Mjini Zanzibar alipokutana na kufanya mazungunzo na Naibu Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Anderew Lentz.

Alisema hatua hiyo inatokana na ukweli kwamba Zanzibar tangu ulipoanza mfumo na uchaguzi wa vyama vingi mwaka 1995 kumekuwa kukijitokeza matatizo wakati wa uchaguzi na kujenga hofu kwa wananchi.

Alisema kutokana na hali hiyo na wakati taifa likelekea kujiandaa kuingia kwenye Uchaguzi Mkuu ni muda mzuri hivi sasa kuwajengea imani wananchi kwa kurekebisha masuala ambayo ndiyo chanzo na chimbuko la kujitokeza hali hiyo.

Othman alisema miongoni mwa masuala hayo ni pamoja na kurekebishwa taratibu na sheria zinazosimamia masuala yote ya mchakato wa uchaguzi Zanzibar, kama ilivyopendekezwa ili mchakato huo kuwa huru na haki.

Othman alisema ni muhimu na ni jambo lisiloepukika katika kufanikisha hali hiyo, viongozi kuhakikisha wanakuwa na dhamira ya kweli ya kisiasa ili kuleta ustawi wa uchaguzi huru na haki kwenye ujenzi wa demokrasia ya vyama vingi.

Alisema kufanya hivyo muhimu na ndio kutathibisha kwamba viongozi wanaweka mbele ustawi wa ujenzi wa amani ya kweli nchini.

Akizungunzia suala la kuwezeshwa vijana katika ajira, alisema kinachohitajika ni kuwepo mfumo wa elimu utakaowaandaa vijana kuwa na maarifa na uwezo wa kitaaluma.

Aidha, alisema kwamba maarifa yataweza pia kuwasaidia vijana kuongeza thamani ya bidhaa wanazozalisha ikiwemo uvuvi wa samaki ambayo wanaweza kuuzwa katika masoko ya ndani na nje ya Zanzibar.

Akizungumzia kuhusu ushirikiano kati ya Zanzibar na Marekani alisema kwamba yapo maeneo mengi yanayoweza kuendelea na ushirikiano huo ikiwa ni pamoja na kuisaidia Zanzibar kuondokana na utegemezi wa nishati ya umeme.

Mengine ni afya, ujenzi wa miundombinu ya barabara pamoja na maendeleo ya biasara katika sekta ya utalii.

Naye Naibu Balozi wa Marekani, Anderew Lentz alisema Marekani inauhusiano wa muda mrefu na Tanzania katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kusisitiza kwamba ni muhumu kwa wananchi kuwa na amani na imani kwenye nchi yao ili kundoa hofu waliyonayo .

Alisema Marekani itaendelea na ushirikiano huo wa muda mrefu katika vipaumbele vya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama vile afya, elimu, miundombinu, utawala bora na uwajibikaji pamoja na mambo mengine mbali mbali.

# GGML yapata ahueni gharama uendeshaji

**Na Mwandishi Wetu, GEITA**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amezindua kituo cha kupokea na kupoza umeme katika Mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGML) chenye uwezo wa megawati 34.

Kituo hicho sasa kitawezesha kampuni hiyo kuanza kutumia umeme wa gridi ya taifa badala ya mafuta, hivyo kupunguza gharama za uendeshaji.

Baada ya kuzindua kituo hicho jana mjini hapa, Dk. Biteko alisema ujenzi wa kituo hicho ni alama halisi ya umoja na ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi kwa kuwa mradi huo umehusisha ujenzi wa laini ya umeme ya kV 33 ambayo imejengwa na TANESCO kwa ya Sh. bilioni 8.04 huku GGML ikijenga kituo cha kupoza umeme kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 24.

Naibu Waziri Mkuu alisema GGML ilikuwa inatumia Sh. bilioni 130 kwa mwezi ambazo ni gharama za uendeshaji na kwenye umeme wa mafuta ilikuwa inatumia Sh. bilioni 13.4 kila mwezi, hivyo kuathiri mapato yake kwa serikali.



Alisema kuanza kazi kwa kituo hicho kutapunguza gharama za uendeshaji kwa mgodi na kuifanya serikali kuongeza mapato, kuongeza ajira na pia GGML kutanua shughuli zake.

Dk. Biteko aliipongeza kampuni hiyo kwa kuanza kutumia umeme wa gridi ambao unapunguza gharama za uendeshaji na kutoa angalizo kuwa kupungua kwa gharama hizo kuendane na kuboresha maslahi ya watumishi.

Alisema umeme mwingi unaozalishwa kwa sasa unatoa uhakika wa kwenda kwa wananchi na watumiaji wakubwa kama GGML na kuweka mkazo kuwa hayo ni matokeo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuijali sekta binafsi.

Sambamba na hayo, alipongeza GGML kwa kuzipa kipaumbele kampuni za wazawa katika kutoa huduma kwenye mgodi huo na kusisitiza kuwa huo ndio msimamo wa serikali wa kuhakikisha kampuni za ndani zinapewa kipaumbele kwenye miradi mbalimbali.

Dk. Biteko aliwaagiza watendaji wa Wizara ya Nishati, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na taasisi zingine za serikali kujali sekta binafsi kutokana na manufaa yake ikiwamo kuwa walipakodi wakubwa na kuongeza ajira.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dk. James Mataragio, alisema hali ya umeme nchini kwa ujumla ni nzuri huku uzalishaji ukikidhi mahitaji na ziada kidogo.

Kuhusu usambazaji umeme mkoani Geita, alisema mkoa una vijiji 486 na kati ya hivyo, 483 vina umeme, sawa na asilimia 99.38.

Alisema kazi ya kupeleka umeme vitongojini mkoani Geita inaendelea na hadi sasa kati ya vitongoji 2,197, takriban 1,000 tayari vina umeme. Alisema mkoa wa Geita umetengewa Sh. bilioni 8.5 kwa ajili ya kupeleka umeme maeneo ya migodi na viwanda na utekelezaji umefikia asilimia 41.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigella, aliishukuru serikali kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji nchini ambayo yamesababisha wawekezaji kufanya kazi na kuletea nchi faida. Alitolea mfano wa miaka mitatu kuwa GGML imezalisha tani 51 za dhahabu jambo ambalo ni mafanikio makubwa yanayochangia ukuaji wa pato la taifa.

Amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha umeme kufika pia kwenye migodi ya wachimbaji wadogo ambayo katika kipindi cha miaka mitatu, wachimbaji wadogo 19 wamepelekewa umeme na kuwezesha uzalishaji wa kilo za dhahabu takriban 11,000.

Makamu wa Rais wa kampuni ya Anglo Gold Ashanti - Tanzania, Simon Shayo, aliishukuru serikali kwa kuweka mazingira mazuri ya biashara na miundombinu madhubuti ya umeme inayowawezesha kufanya biashara kwa ufanisi.

Amesema mradi huo ni muhimu kwa GGML kwa kuwa unawawezesha kupata umeme wa gridi na kupunguza matumizi ya umeme wa mafuta na gharama zitapungua kwa asilimia 92.

# Sekta za serikali zabanwa kulipa kodi

**Na Christina Haule, MOROGORO**

WADAU wa sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi nchini wametakiwa kujenga tabia ya kulipa kodi kwa hiyari ili kuepuka adhabu na faini.

Ofisa Mkuu Msimamizi wa Kodi Upande wa Elimu na Mawasiliano wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), jijini Tanga, Flavian Byabato, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kilele cha maadhimisho ya sherehe za Maonesho ya Wakulima Nanenane, Kanda ya Mashariki yaliyofanyika eneo la Tungi nje kidogo ya Manispaa ya Morogoro.

"Mfugaji, mkulima au mvuvi, wote tuwaite wakulima ambapo wana nafasi ya kulipa kodi pale anapofanya kilimo kibiashara sababu ni pato la kiuchumi, pia wapo watu wananunua mazao na kuuza, kwa mauzo yoyote ya kibiashara yanayoleta kipato kuanzia Sh. milioni nne na kuendelea kwa mwaka yanaingia kwenye wigo wa kulipiwa kodi ya mapato," alisema.

Alisema vipo viwango vya ulipaji vimewekwa kisheria ili kumfanya mkulima kupata nafasi ya kulipa kodi kuanzia mwenye mapato ya Shilingi milioni nne hadi saba kiwango cha kodi ni Sh. 100,000 na mwenye mapato ya Shilingi milioni saba hadi 11 ni Sh. 250,000, hela inayozidi huwa ni asilimia 3.5 ya mauzo yote kwa mwaka mzima huku mauzo ya chini ya Shilingi milioni nne yakiingia kwenye msamaha wa kodi.

Alisema TRA imekuwa ikitoa elimu kwa wakulima kwa kuwafikia kwenye maeneo yao ikiwamo kwenye maonesho hayo ili kuwaweka katika njia za ulipaji kodi.

Alitoa wito kwa wakulima na wananchi kwa ujumla kuendelea kuwa na uhiyari wa kulipa kodi kwasababu inayokusanywa hujenga miradi ya kimkakati nchini kama ilivyofanya kwa SGR, Bwawa la Mwalimu Nyerere, barabara na miundombinu mingine.

Naye Ofisa Mwandamizi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi, Immaculete Chaggu, aliwataka wakulima kuzingatia masuala ya ulipaji kodi kwa sababu tayari serikali imeshatoa msamaha kwa kiasi kikubwa kwenye bidhaa za kilimo, mifugo na uvuvi na kuleta wepesi kwenye kilimo.

Chaggu alisema wakulima wengi wanakimbilia kufanya biashara bila kujua kutunza kumbukumbu na kuingiza fedha za kilimo kwenye biashara zingine na kuvuruga utaratibu wao wa makusanyo.

Aliwashauri wafanyabiashara kwenye sekta ya kilimo, uvuvi na ufugaji kutunza kumbukumbu zao za kibiashara zikiwamo risiti za mauzo na ununuzi kwa kuwa husaidia kukokotoa makisio ya kodi ya mapato ambayo mfanyabiashara atalipa kwa mwaka husika.

Alisema, kumbukumbu hizo humsaidia kujua mwenendo wa biashara yake kama inakua au la.


## TANGAZO LA MNADA

**Freemind, Held, Marmboto** Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya Mnada Jijini Dar es salaam Mteja anashauriwa kulipa deni ndani ya siku 14 za hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe ya Mnada inavyoonekana hapa chini.

| | Client name | Aina ya gari | Auctioneer | Tarehe ya Mnada |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Aggrey Sebauth Mwanyombole | Toyota Corolla T428DDR | Held | 29.08.2024 |
| 2 | Agness Michael Junga | Nissan Dualis-T858EJG | Freemind | 29.08.2024 |
| 3 | Athuman Juma Farijala | Daihatsu MIRA T275EBE | Marmboto | 29.08.2024 |
| 4 | Ruth Solomon Mwaipyana | Subaru Forester T822DCR | Marmboto | 29.08.2024 |
| 5 | Raphael Costantine Bandiho | Toyota Landcruiser T578AVX | Freemind | 29.08.2024 |

**Masharti ya Mnada.**

1. Mnunuzi atakaye shinda atalipa 25% (au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la 75% litalipwa ndani ya siku kumi nne (14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa muda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo.

Kwa Mawasiliano Piga 0677014355 (Fanikiwa)

## TANGAZO GARI LINAUZWA

Gari aina ya **TOYOTA HILUX** lenye namba za usajili **T164DXV** linauzwa lipo katika hali nzuri.

**Taarifa za Gari**

Aina ya gari: **Toyota Hilux**
Mwaka wa kutengenezwa gari: **2004**
Mafuta inayotumia: **Diesel**
Model Namba: **KF-LN167**
Uwezo wa injini: **2980**
Aina ya bodi: **Station Wagon**
Rangi ya gari: **Multi Colour**
Chesesi namba: **LN1670032032**
Namba ya injini: **5L5506667**
Kilometa ilizotembea: **110197**








KWA MAWASILIANO ZAIDI
Piga: 0757823350 / 0692793423

## KUPOTEA KWA CHETI




**EMMANUEL AUGUSTINE WEMA**. ANATANGAZA KUPOTEA KWA CHETI CHA KIDATO CHAKE CHA KIDATO CHA NNE KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI MWAKA 2018 URU SEKONDARI ILIYOKO KILIMANJARO WILAYA YA MOSHI CHENYE INDEX NO **S0357.0071.2018** . KWA YEYOTE ATAKAYEKIONA ANAOMBWA KUTOA TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA :- **PHQ/ARU/ARU/27288/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI


**JOHNSON JONATHAN MBASHA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye jina la umiliki **CONNECTION INVESTMENTS (T) LTD** yenye namba ya usajili **T 536 DYF,** CHASSIS NAMBA: **KJ10201204** na ENGINE NAMBA: **MR206356684.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/149034/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**NEEMA AMANYISYE KALESI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0214/0048** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MSALATO SECONDARY SCHOOL** mwaka 2010. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/TEM/169549/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**RICHARD JOSEPH** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P.0458/0026** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KASULU TEACHER'S COLLEGE** mwaka 2002. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **SO/RB/6248/2017**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SYLIVESTER MICHAEL KIRWANDA** anatangaza kupotea kwa cheti cha darasa la saba chenye index namba: **PS1404033-036** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia SHULE YA MSINGI YA KIGAMBONI mwaka 2017. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **MAF/REF:9910838343198.**

HABARI KIMATAIFA

# Iran yapuuza wito kutoishambulia Israel

**TEHRAN,** IRAN

IRAN imepuuzia wito wa mataifa ya magharibi wa kuacha vitisho vyake vya kulipiza kisasi dhidi ya Israel kwa mauaji ya kiongozi wa kisiasa wa kundi la Hamas, Ismail Haniyeh, yaliyofanyika siku chache zilizopita katika ardhi ya taifa hilo.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Iran, Nasser Kanaani, alisema jana kuwa wito wa Ufaransa, Ujerumani na Uingereza hauna mantiki, wala mashiko ya kisiasa na unakinzana na kanuni za sheria za kimataifa.

Kwa mujibu wa kanuni, wito wa mataifa hayo ambao haukulaani uhalifu wa kimataifa unaofanywa na Israel, unaitaka Iran isichukue hatua zozote za kuizuia Israel ambayo imekiuka uhuru wa mamlaka ya eneo lake.

Alisema Iran imedhamiria kuzuia mashambulizi ya Israel na kutoa wito kwa Ufaransa, Ujerumani na Uingereza kupinga vita vya Gaza na Israel ambayo inachochea vita.

"Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kutochukua hatua na uungaji mkono mkubwa wa kisiasa na kijeshi wa serikali za Magharibi kwa utawala wa Israel, ndiyo sababu kuu zinazoufanya mzozo wa Gaza kutanuka na kuwa wa kikanda," alisema Kanaani.

Aliongeza kuwa Marekani na washirika wake wa Ulaya ziliitolea wito Iran na washirika wake kujizuia na mashambulizi dhidi ya Israel na kuepusha kutanuka kwa mzozo.

Aidha, ilielezwa kuwa Iran na washirika wake makundi ya Hamas na Hezbollah la Lebanon, wameishutumu Israel kwa kufanya mauaji ya Haniyeh. Licha ya kwamba serikali ya Israel haijakiri kuhusika na mauaji hayo.

Wakati huo huo, ilielezwa kuwa wanajeshi wa Israel wamemuua kwa kumpiga risasi mwanaume wa Kipalestina wakati wa msako mkali wa kuvunja makaazi ya washukiwa wawili wa Kipalestina waliokuwa wamezuiliwa jana alfajiri katika Ukingo wa Magharibi, kwenye miji ya Ramallah na Al-Bireh.

Jeshi la Israel halikuweza kuthibitisha mara moja taarifa hizo zilizotolewa na maofisa wa Wizara ya Afya ya Palestina, pamoja na shirika la habari la Kipalestina la Wafa, ingawa ilisema inazifuatilia kwa undani.


Shirika linalofuatilia wafungwa wa Kipalestina, lilisema kuwa mwanaume huyo aliyeuawa mwenye umri wa miaka 18, aliachiliwa huru Novemba 25, wakati wa makubaliano ya kusitisha mapigano kwa wiki moja.

Alisema katika hatua hiyo pia Wapalestina wengi waliachiliwa huru kutoka kwenye magereza ya Israel na kubadilishana mateka wa Israel waliokuwa wakishikiliwa huko Gaza tangu Oktoba 7.

Katika hatua nyingine, Wizara ya Afya ya Palestina ilisema vikosi vya Israel vilimuua mwanaume mwingine wa Kipalestina karibu na mji wa Azzun mashariki mwa mji wa Qalqilya.

Jeshi la Israel lilisema kuwa awali mwanaume huyo alimfyatulia risasi raia wa Israel huko Qalqilya. Huku Hamas ikisema kijana huyo alikuwa mmoja wa wapiganaji wake.

***(DW, AFP, DPA, Reuters)***



Wakazi wa Sudan waliokosa makazi kutokana na mapigano kati ya jeshi na wanamgambo wa (RSF). **PICHA: MTANDAO**

# FBI kuchunguza udukuzi wa Iran

**WASHINGTON,** MAREKANI

SHIRIKA la Ujasusi la Marekani (FBI) limeanzisha uchunguzi kuhusu madai kuwa kambi ya kampeni ya Trump ililengwa na wadukuzi wanaofanya kazi kwa ajili ya serikali ya Iran.

Hayo ni kwa mujibu wa taarifa ya shirika hilo iliyotolewa jana, ikisema kuwa FBI inachunguza suala hilo bila kumtaja rais wa zamani au Iran.

Msemaji wa kambi ya kampeni ya Trump aliiambia BBC kuwa hati hizo zilipatikana kinyume cha sheria na vyanzo vya kigeni vinavyoichukia Marekani.

Maofisa wa Iran walikanusha kuhusika na udukuzi huo na serikali ya Marekani haijaishutumu rasmi Iran juu ya suala hilo. Huku jarida la CBC News likibainisha kuwa FBI inachunguza kama wadukuzi wa Iran walilenga kambi ya Joe Biden na Kamala Harris pia.

Taarifa ya kambi ya kampeni ya Trump ilitolewa siku moja baada ya Microsoft kutoa ripoti inayoonyesha kwamba wadukuzi wa Iran walilenga kampeni ya mgombea urais wa Marekani ambaye hakutajwa jina mwezi Juni.

Siku chache zilizopita Trump alisema wadukuzi waliweza kupata habari zilizokusudiwa kutolewa kwa umma.

Kwa mujibu wa gazeti la Washington Post, wafanyakazi watatu wa kambi ya kampeni ya Biden-Harris pia walilengwa na barua pepe za ulaghai siku chache kabla ya Rais Joe Biden kutangaza kwamba anajiondoa kwenye kinyang'anyiro cha kuingia ikulu kwa mhula wa pili.

Msemaji wa kambi ya kampeni ya Harris alisema katika taarifa yake kwamba wanafuatilia kwa uangalifu na kuhakikisha ulinzi dhidi ya vitisho vya mtandao, na kwamba hawafahamu ukiukaji wowote wa usalama wa mifumo yao.

***BBC***

## Zambia, DRC zafungua mpaka baada ya siku kadhaa

**KINSHASA,** DRC

MPAKA wa Kasumbalesa kati Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Zambia umefunguliwa tena baada ya kufungwa kwa muda wa siku tatu hali iliyosababisha adha na msongamano mkubwa wa magari yanayotumia mpaka huo.

Ilielezwa kuwa kituo hicho cha mpakani ni cha pili kwa umuhimu nchini DRC baada ya Kinshasa. Na kwamba uamuzi wa kufunguliwa upya ulichukuliwa juzi Jumatatu mjini Lubumbashi kufuatia mkutano kati ya waziri wa Biashara wa Kongo na mwenzake wa Zambia.

Waziri wa Biashara na Viwanda wa Zambia, Chipoka Mulenga alisema kwamba kuanzia saa 6:00 asubuhi mpaka kati ya DRC na Zambia utakuwa wazi tena, huku akisisitiza juu ya kuheshimu mikataba ya kibiashara inayowahusu pande zote mbili.

"Kwa miaka kadhaa, DRC na Zambia zilitia saini mkataba wa kibiashara, ni muhimu sana kurejelee makubaliano hayo kila wakati kama walivyofanya. Nimefurahi sana kwa sababu bidhaa za Zambia zitaingia DRC bila vikwazo vyovyote," alisema.

Ilielezwa kuwa juzi Zambia ilifunga vituo vitatu vya mpaka na DRC kupinga uamuzi uliochukuliwa Julai wa kupiga marufuku uingizaji wa bia na vinywaji baridi kutoka nje ya nchi.

Waziri wa Biashara wa Kongo, Julien Paluku alieleza kuwa DRC haijakiuka makubaliano hayo. Na kwamba marufuku ya bia na vinywaji baridi inahusu bidhaa kutoka nchi zingine.

"Bidhaa tu ambazo ni kutoka Zambia ndizo zinazonufaika na fursa. Na ninawaambie kuwa usafirishaji katika nchi zote zinazotuzunguka husababisha DRC kupoteza karibu dola bilioni 5 kila mwaka," alisema.

Ilielezwa kuwa nchi hizo mbili zilikubaliana kuunda tume ya pamoja ya kuhakiki asili ya bidhaa kabla ya kuvuka mpaka.

***RFI***

**"Kwa miaka kadhaa, DRC na Zambia zilitia saini mkataba wa kibiashara, ni muhimu sana kurejelee makubaliano hayo kila wakati kama walivyofanya. Nimefurahi sana kwa sababu bidhaa za Zambia zitaingia DRC bila vikwazo vyovyote," alisema.**

# SIMBA QUEENS KUWANIA TAJI LA CECAFA

Na Somoe Ng'itu

KIKOSI cha Simba Queens kinatarajia kuondoka nchini leo kuelekea Ethiopia kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), yanayotarajiwa kufanyika nchini humo kuanzia Jumamosi, imeelezwa.

Simba Queens ilikata tiketi ya kushiriki mashindano hayo baada ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL).

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Simba Queens, Selemani Makanya, alisema maandalizi kuelekea mashindano hayo yamekamilika na kikosi chao kimejipanga kwenda kutwaa ubingwa wa michuano hiyo.

Makanya alisema lengo la Simba Queens ni kutwaa taji la Afrika, hivyo wanakwenda Ethiopia kupambana na hatimaye kupata tiketi ya kuiwakilisha CECAFA katika Fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake zitakazofanyika baadaye mwaka huu.

"Kila kitu kinakwenda vizuri, mimi (Makanya nitaondoka kesho (leo) lakini kikosi kamili kitaondoka Jumatano, tumejiandaa vizuri kwa sababu tunajua ni mashindano yanayoshirikisha mabingwa wa kila nchi kutoka kwenye ukanda wetu, tunaenda kuilinda na kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania," Makanya alisema.

Aliongeza kila mechi kwao itakuwa muhimu na hawatawadharau wapinzani wao kuanzia mechi ya kwanza watakaocheza Jumapili dhidi ya FAD kutoka Djibouti.

"Kila mechi kwetu ni sawa na fainali, tunataka kuendeleza mazuri tuliyoyafanya katika ligi kwenye msimu uliomalizika, hatutaki kwenda kushiriki, tunaenda Ethiopia kupambana, tunajua hakuna mechi rahisi katika mashindano haya ya CECAFA na hata yale ya Afrika," alisema Makanya.

Nahodha wa timu hiyo, Violeth Nicolas, aliliambia gazeti hili wachezaji wote wako katika hali nzuri na wanaenda Ethiopia kupambana.

"Tumejiandaa vizuri, tunataka kurejea nyumbani na taji la CECAFA, hii ndio itakayotupa tiketi ya kwenda katika fainali za Afrika," alisema nahodha huyo.

Simba ambayo imepangwa katika Kundi B itashuka tena dimbani Agosti 20, mwaka huu kuvaana na Kawempe Muslim FC kutoka Uganda na itamaliza mechi za hatua ya makundi dhidi ya mabingwa wa Burundi, PVP Buyenzi siku mbili baadaye.

Timu mbili zitakazomaliza katika nafasi mbili za juu zitatinga hatua ya nusu fainali na fainali ya mashindano hayo itafanyika Agosti 21, mwaka huu.



Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis (wa tatu kulia), akiongozana na Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo (kulia kwake), kwenye ufunguzi wa bonanza la mazoezi ya mwili lilioandaliwa na Balozi wa Mazingira, Grit Mwimanzi (wa pili kulia), kwa kushirikiana na Umoja wa Vilabu vya Mazoezi Kata ya Vingunguti (UVIJOVI) lililofanyika Viwanja vya Msikate Tamaa, Vingunguti jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## JKT Tanzania yakomalia safu yake ya ushambuliaji

Na Shufaa Lyimo

BENCHI la ufundi la timu ya JKT Tanzania limesema linaendelea kuimarisha safu yake ya ushambuliaji kuiongozea makali ili iweze kutumika kwa usahihi nafasi watakazokuwa wakizitengeneza.

JKT wanatarajia kufungua pazia la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2024/2025 kwa kuanza kucheza na Azam FC Agosti 28 mwaka huu kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuyo, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Hamady Ally, alisema kwa sasa ana kazi moja ya kuipa mbinu safu hiyo kwa lengo la kupata pointi tatu katika kila mchezo.

"Sasa hivi naendelea kutoa mbinu mbadala kwenye safu yangu ya ushambuliaji ili tupate matokeo mazuri katika mchezo wetu wa kwanza dhidi ya Azam FC," alisema Ally.

Kocha huyo alisema anafurahishwa na muunganiko mzuri uliopo kwa wachezaji wake uwanjani, lakini ushirikiano mzuri kutoka kwa viongozi na anaamini umoja huo utaleta mafanikio makubwa msimu ujao.

Aliongeza kuwa hana wasi wasi kukutana na Azam FC kwa kuwa ana kikosi kizuri ambacho anakiamini kwa asilimia 100.

Alisema kwa sasa anaendelea kuyafanyia kazi mapungufu ambayo aliyabaini kwenye michezo ya kirafiki waliyocheza mkoani Mbeya ili kukiimarisha zaidi kikosi chake.

Aidha, aliomba mashabiki wao waendelee kuwapa ushirikiano ili waweze kutimiza malengo yao ya kushika nafasi za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu msimu huu.



# Maxime: Dodoma Jiji FC tuko tayari

Na Somoe Ng'itu

KOCHA Mkuu wa Dodoma Jiji, Mecky Maxime, amesema hataongeza mchezaji yeyote kwa sasa na kikosi chake kiko tayari kwa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaofanyika kuanzia keshokutwa.

Dodoma Jiji itaanza kampeni zake za kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara ugenini Jumamosi dhidi ya wenyeji Mashujaa FC kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

Maxime alisema wachezaji wake wameimarika na anaamini wataanza vyema msimu mpya kwa kupata matokeo chanya.

"Tuko tayari kwa ajili ya msimu mpya, nimeridhishwa na kiwango cha wachezaji wangu na kwa sasa sina mpango wa kuongeza mchezaji katika siku chache zilizobakia kabla ya dirisha la usajili kufungwa," alisema Maxime.

Aliongeza wamejipanga kukutana na ushindani katika msimu mpya kwa sababu timu zote 16 zitakazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara zimefanya usajili mzuri na zimejiandaa vyema.

Yanga ndio mabingwa watetezi wa ligi hiyo wakati Azam FC ilimaliza katika nafasi ya pili ikifuatiwa na Simba.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### COMAN ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL inapanga kumsajili winga Mfaransa, Kingsley Coman, kwa mkopo kwa msimu huu, huku Bayern Munich ikiwa tayari kumruhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kuondoka. ***(Football Insider)***

### TONEY AWINDWA SAUDIA

MSHAMBULIAJI wa Brentford, Ivan Toney anaangaliwa na klabu za Saudi Pro League, huku Al-Ahli wakimtaka nyota huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 28. ***(Fabrizio Romano)***

### PSG YAMTAKA PARRIS

KLABU ya Newcastle United inalenga kumnunua mshambuliaji wa Manchester United, Nikita Parris, mwenye umri wa miaka 30, huku wakitarajia kupandishwa kwenye Ligi Kuu ya Wanawake. ***(Guardian)***

### BROJA ANUKIA STUTTGART

STUTTGART iko katika mazungumzo ya kumsajili, Armando Broja, kwa mkopo kutoka Chelsea, huku mshambuliaji huyo wa Albania mwenye umri wa miaka 22 akiwa tayari kujiunga na klabu hiyo ya Ujerumani. ***(Sky Sports Ujerumani)***

### ABRAHAM ATAJWA AC MILAN

AC Milan inataka kumsajili kwa mkopo na chaguo la kumnunua mshambuliaji wa AS Roma, Tammy Abraham, mwenye umri wa miaka 26, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Bournemouth, Everton na Leicester City. ***(Calciomercato)***

### FOREST YAIBANIA ATALANTA

KLABU ya Nottingham Forest imekataa ombi la Atalanta la zaidi ya euro milioni 20 kumnunua beki wa Wales, Neco Williams, mwenye umri wa miaka 23. ***(Fabrizio Romano)***

### VAN DIJK MAMBO MAGUMU

MLINZI wa Liverpool, Virgil van Dijk, amesalia na mwaka mmoja katika mkataba wake na Wekundu hao na mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 33 amesema hakuna mabadiliko yoyote katika mkataba huo. ***(Liverpool Echo)***

### EDERSON KUBAKIA CITY

GOLIKIPA wa Brazil, Ederson, mwenye umri wa miaka 30, amekuwa akihusishwa na kuhamia Saudi Arabia, lakini amesema anasalia Manchester City baada ya mazungumzo na Kocha Pep Guardiola. ***(Mirror)***

### LOANNIDIS SOKONI RASMI

LEICESTER City imetuma dau la pauni milioni 23.2 ili kumnunua mshambuliaji wa Panathinaikos na Ugiriki, Fotis Loannidis, mwenye umri wa miaka 24 huku wakiendelea na mazungumzo ya kujaribu kumnunua winga wa Ivory Coast, Wilfried Zaha (31), kutoka Galatasaray. ***(Telegraph)***

### CAJUSTE ANUKIA BRENTFORD

BRENTFORD imekubali dili la kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Sweden, Jens Cajuste kutoka Napoli kwa mkopo wa msimu mzima, na ahadi ya kumnunua jumla kwa dau la takriban pauni milioni 10. ***(Football Insider)***

### BEIER KUTUA DORTMUND

KLABU ya Borussia Dortmund inatazamia kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Maximilian Beier, mwenye umri wa miaka 21 kutoka Hoffenheim kwa mkataba wa thamani ya zaidi ya euro milioni 30. ***(Sky Sports)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VINICIUS JR AKATAA OFA KUTUA SAUDIA

Mbrazil huyo afunguka anahitaji kushinda Ballon d'or akiwa...

**MADRID, Hispania**

VINICIUS Juniorameripotiwa kukataa ofa kutoka kwa Ligi Kuu ya Saudi Arabia (Saudi Pro League), kwa ajili ya kuendeleza ndoto yake ya kushinda Ballon d'Or akiwa na Real Madrid.

Winga huyo amekuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani kwa misimu mitatu iliyopita, baada ya kusajiliwa na Madrid akiwa na umri wa miaka 16 tu, halafu akahamia Hispania akiwa na umri wa miaka 18.

Lakini kwa kuwa Ligi ya Saudia inataka kuendelea kujitangaza na kuvutia wachezaji wa hali ya juu katika kilele cha maisha yao ya soka, nyota huyo wa Brazil amekuwa akilengwa.

Mfuko wa Uwekezaji wa Umma wa Saudi Arabia (PIF) unadhibiti klabu nne kubwa nchini humo ambazo ni Al Hilal, Al Ittihad, Al Nassr na Al Ahli, gazeti la The Athletic limeandika mjumbe wa PIF, kaimu kwa niaba ya Wizara ya Michezo, aliwasiliana na wawakilishi wa Vinicius.

Matumaini yao ni kumfanya mchezaji huyo kuwa uso wa Saudi Pro League katika maandalizi ya Kombe la Dunia la mwaka 2034, ambalo litaandaliwa na taifa hilo la ghuba.

Haki za uenyeji hazijatolewa rasmi na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), lakini ombi la Saudi Arabia halijapingwa.

Lakini Vinicius amezungumzia kuhusu uvumi huo akisema ana furaha kuwa Madrid, ambapo ana mkataba hadi mwaka 2027.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 pia ana kipengele cha kuachiliwa cha euro bilioni moja.

Kwa sasa, bado hajamalizana na matarajio yake barani Ulaya na haswa akiwa na Real Madrid, ambayo ni pamoja na kushinda tuzo ya Ballon d'Or wakati akiichezea klabu hiyo maarufu.

Lakini Saudi Arabia haitarajiwi kukataa kwa jibu na inapendekezwa kuanzisha upya nia yao katika siku zijazo.

Saudi Pro League imetatizika kuondoa lebo za kile kinachoitwa ‚ligi ya kustaafu'. Cristiano Ronaldo ameshuhudia ufungaji wake ukiongezeka tangu ahamie huko lakini atasherehekea kutimiza miaka 40 msimu huu.

Neymar alikubali ofa hiyo akiwa na umri wa miaka 31, sawa na Sadio Mane. Riyad Mahrez na N'Golo Kante walikuwa na umri wa miaka 32, Karim Benzema alikuwa ana umri wa miaka 35, wakati wachezaji wengine wenye hadhi ya juu - kama vile Franck Kessie, Ruben Neves na Aleksandar Mitrovic - hawafikii kwenye ‚daraja la dunia'.

Katika majira ya joto ya 2023, Al Hilal walitoa ofa ya rekodi ya dunia ya euro milioni 300 kwa Kylian Mbappe, ambayo Paris Saint-Germain ilikubali kwa furaha, lakini mchezaji huyo alikataa hata kukutana na klabu.

Saudi Arabia imetumia kiasi kikubwa cha fedha kujaribu kujitangaza kama kitovu cha michezo.

HABARI MICHEZO

# CARVALHO ATIMKA LIVERPOOL




**LIVERPOOL,** ENGLAND

BRENTFORD imesajili kiungo mkabaji, Fabio Carvalho, kutoka Liverpool kwa mkataba wa miaka mitano, klabu hiyo ya London Magharibi ilitangaza jana.

Taarifa za kifedha hazikufichuliwa lakini vyombo vya habari vya England viliripoti mkataba huo ulikuwa na thamani ya karibu pauni milioni 27.5.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 aliiwakilisha England katika ngazi mbalimbali za vijana kabla ya kuhamia Ureno, ambako alizaliwa na kuitumikia timu ya vijana ya umri chini ya miaka 21.

Alijiunga na Liverpool mwaka 2022 akitokea Fulham.

Carvalho, ambaye msimu uliopita alicheza kwa mkopo katika klabu ya RB Leipzig ya Bundesliga na Hull City, aliichezea Liverpool mechi 21 katika michuano yote, akifunga mabao matatu.

Alifunga pia katika ushindi wa maandalizi ya msimu dhidi ya Arsenal na Manchester United msimu huu wa joto.

Mapema Jumatatu, klabu ya Serie ya A ya AC Milan walikuwa wamemsajili beki wa Brazil, Emerson Royal kutoka Tottenham Hotspur kwa mkataba utakaomalizika Juni, 2028 na chaguo la kuongezwa kwa mwaka mmoja.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 25, alicheza mechi 10, alijiunga na Spurs mwaka 2021 akitokea Barcelona ya Hispania.

Pia aliwahi kucheza Atletico Mineiro ya Brazil, baada ya kuanza maisha yake ya ujana katika klabu ya Ponte Preta.

Emerson, ambaye aliichezea Spurs mechi 101 katika mashindano yote, atavaa jezi nambari 22 akiwa Milan.

## De Ligt, Mazraoui kutua Man United

**MANCHESTER,** ENGLAND

WACHEZAJI Matthijs de Ligt na Noussair Mazraoui wanakaribia kuwa wachezaji wa Manchester United baada ya wote kuonekana kwenye viunga vya timu hiyo kwa ajili ya vipimo vya afya baada ya kuondoka Munich.

United imefikia makubaliano ya uhamisho wa wachezaji hao wawili na Bayern Munich yenye thamani ya hadi pauni milioni 60 ambayo wanatumaini itaimarisha safu ya ulinzi ambayo ilikumbwa na majeraha msimu uliopita na imeendelea kuathiri maandalizi ya kampeni mpya ya 2024/2025.

Mkataba huo pia unaahidi kuruhusu Bayern Munich kuendelea na usajili wao, huku beki wa kati wa Bayer Leverkusen, Jonathan Tah, baada ya kufikia hatua ambayo walihitaji kuwaondoa wachezaji kabla ya kusajiliwa tena.

Wawili hao sasa wameingia England na wanatarajiwa kukamilisha taratibu ambazo hazijakamilika za mchakato wa uhamisho.

Baada ya kumwachilia Raphael Varane mwishoni mwa msimu uliopita, United tayari wametumia fedha nyingi kumnunua beki wa kati, Leny Yoro, mwenye umri wa miaka 18 msimu huu wa joto.

Lakini alipata jeraha la mguu wakati wa mechi yake ya pili ya kujiandaa na msimu mpya na kuhitaji kufanyiwa upasuaji.

Mazraoui atashindana na Diogo Dalot kuwania nafasi ya beki wa kulia, ingawa wachezaji wote wawili wana uwezo wa kufanya kazi upande wa kushoto, ambapo Luke Shaw alikosa sehemu kubwa msimu uliopita na Tyrell Malacia hakuwapo kwa kipindi chote cha kampeni.

Hakuna beki wa kushoto aliyekuwapo kwenye kikosi cha Ngao ya Jamii mwishoni mwa wiki, huku Erik ten Hag alilazimika kumtumia Harry Amass wa miaka 17 kwenye mchezo huo dhidi ya Manchester City pale kwenye dimba la Wembley.

## Durant anunua hisa za PSG

**PARIS,** UFARANSA



NYOTA wa mpira wa kikapu wa Marekani, NBA, Kevin Durant, amekuwa mwanahisa mpya wa miamba wa Ligi Kuu Ufaransa maarufu Ligue 1, Paris Saint-Germain, klabu hiyo ya Ufaransa imetangaza.

Mshindi wa medali ya dhahabu ya hivi majuzi katika michezo wa Olimpiki akiwa na Timu ya Marekani amewekeza mamilioni ya fedha zake ili kujiunga na klabu hiyo, chanzo kiliiambia ESPN.

Alifanya hivyo kupitia Arctos Sports Partners, mfuko wa uwekezaji wa Marekani ambao ulinunua hisa za asilimia 12.5 katika klabu hiyo mwaka 2023 kwa PSG yenye thamani ya dola bilioni 4.6.

Madhumuni ya ujio wa Durant katika klabu hiyo ni kuendeleza zaidi chapa ya PSG nchini Marekani kutokana na mtazamo wa masoko na udhamini, hasa michuano ya Klabu bingwa ya Dunia 2025 na Kombe la Dunia la 2026.

Durant mwenye umri wa miaka 35 anayechezea Phoenix Suns, ni shabiki mkubwa wa soka na sehemu ya mmiliki wa klabu ya MLS ya Philadelphia Union.

Yeye ni rafiki mkubwa wa Rais wa PSG, Nasser Al Khelaifi, na ametembelea uwanja wa mazoezi wa Paris na uwanja wa Parc des Princes mara kadhaa kabla ya uwekezaji wake.

Agosti 6 alienda kwenye akademi ya PSG kuwasalimu baadhi ya wachezaji, wafanyakazi na kocha mkuu, Luis Enrique.

Durant anafurahi sana kujihusisha na PSG, chanzo kiliiambia ESPN, na yuko makini sana kuhusu uwekezaji wake katika klabu.

HABARI MICHEZO

# BEKI ISRAEL MWENDA ATIMKA SIMBA RASMI

**Na Faustine Feliciane**

BEKI wa pembeni wa klabu ya Simba, Israel Mwenda, rasmi ametangaza kuachana na klabu hiyo kwa makubaliano ya pande mbili, imefahamika.

Nyota huyo ambaye kwa muda mrefu alihudumu kama beki chaguo la pili kwenye kikosi cha Simba nyuma ya Shomari Kapombe.

Katika mtandao wake wa kijamii, beki huyo aliandika taarifa ya kuishukuru na kuiaga timu hiyo kwa muda wote aliokuwa akiitumikia klabu hiyo.

Alipoulizwa Menaja wa Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, juu ya taarifa ya beki huyo kuachana na Simba, alisema ni kweli lakini nyota huyo aliomba mwenyewe kuondoka kwa kuwa amepata timu nyingine.

„Mwenda tumemruhusu leo (jana) baada ya yeye mwenyewe kuomba kuondoka kwa madai amepata timu nyingine,“ alisema Ahmed.

Aidha, alisema kuwa mchezaji huyo jana alilipa kiasi cha fedha alichotakiwa kurudisha baada ya kusaini mkataba mpya hivi karibuni.

„Tumempa barua ya kumwachia na sasa yupo huru, klabu inamtakia kila la heri huko anakokwenda,“ alisema Ahmed.

Awali, Mwenda aliomba kuachana na klabu hiyo siku chache baada ya kusaini mktaba mpya huku akiwa amelipwa stahiki zake za kusaini mkataba huo.

Uongozi wa Simba ulikubaliana naye kwa sharti la kurudisha fedha alizochukua kwenye mkataba mpya.

Katika hatua nyingine, taarifa zinadai beki huyo yupo kwenye mazungumzo ya kutaka kujiunga na klabu ya Singida Black Stars ambapo anaamini atapata nafasi ya kucheza mara kwa mara.



Baadhi ya wachezaji wa Simba Queens wakiwa kwenye mazoezi ya mwisho jana kabla ya leo kuanza safari kuelekea Ethiopia kwenye mashindano ya Mabingwa Afrika Mashariki na Kati kusaka tiketi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake. **PICHA: SIMBA**

# Namungo kuiwahi Fountain Gate

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Namungo ambayo ipo jijini Dar es Salaam, imesema inajiandaa kuwahi mkoani Lindi kuipokea Fountain Gate kwa ajili ya mchezo wao wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaopigwa Jumamosi, Uwanja wa Majaliwa, Rungwa mkoani Lindi.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Shadrack Nsajigwa, alisema wanataka kuwahi mapema kurejea Lindi kwa ajili ya maandalizi yao ya mwisho kabla ya mchezo huo.

Alisema anaenda kukutana na timu hiyo huku wakiwa tayari wamekutana kwenye mchezo wa kirafiki uliochezwa hivi karibuni wilayani Karatu.

“Tumepata ‚pre seasons‘ nzuri tu kule Karatu, kwa sasa naona wachezaji wapo timamu, katika mechi zetu tano za kirafiki moja wapo tulicheza na Fountain Gate kwa hiyo imekuwa kama bahati kukutana nayo tena katika mechi ya ufunguzi, ingawa kwenye maandalizi kujua kiwango halisi cha timu yenyewe ni ngumu lakini nimepata mawili matatu, naamini msimu huu utakuwa mzuri kuliko uliopita,“ alisema Nsajigwa.

Naye mchezaji wa timu hiyo, Erasto Nyoni, alisema maandalizi yao yamekwenda vyema, akiwa na imani kuwa msimu ujao timu yao itashika nafasi ambazo itastahili baada ya kushindwa kufanya hivyo msimu uliopita.

“Kama unakumbuka Namungo imeshawahi hata kucheza mechi za kimataifa, lakini kwa sasa imerudi nyuma kidogo, ila tumefanya usajili ambao utatusaidia kuirejesha kwenye makali yake yaliyozoeleka,“ alisema Nyoni.



## Mambo yawageukia Magoma, mwenzake

INATOKA UK. 24

Gamondi, alisema anafahamu umuhimu na faida ya kucheza kwenye uwanja wa nyumbani, lakini watamuheshimu mpinzani wao kwa kuwa soka ni mchezo wenye matokeo ya kushangaza wakati mwingine.

“Tunajiandaa kikamilifu, mchezo hautakuwa mwepesi kama inavyodhaniwa, najua wapinzani wetu licha ya kucheza hapa Tanzania michezo yote, wamejiandaa vizuri, tutakabiliana nao kwa tahadhari,” alisema Gamondi.

Yanga wanatarajia kuumana na Vital'O, Agosti 17 kwenye mchezo wa kwanza ambao Warundi hao watakuwa wenyeji kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi kabla ya kurudiana wiki moja baadaye Uwanja wa Benjamin Mkapa ambao Yanga watakuwa wenyeji.

## Rekodi za nyota mpya Simba

INATOKA UK. 24

kupatikana mabao mawili.

Inaelezwa ujio wa nyota huyo ni mapendekezo na kocha wa klabu hiyo, Fadlu davids ambaye alitaka viongozi kuongeza mshambuliaji mwingine haraka iwezekanavyo.

Kutua kwa nyota huyo kunamaanisha sasa mshambuliaji Fred Michael na golikipa Ayoub Lakred ambaye yupo nje akiuguza majeraha mmoja wapo atampisha Mcameroon huyo kwenye orodha ya wachezaji wa kimataifa watakaoutumiwa msimu huu.

Mmoja wa viongozi ndani ya klabu hiyo aliiambia Nipashe kuwa kuna uwezekano mkubwa jina la Lakred likaondolewa kwenye orodha ya wachezaji watakaotumiwa msimu huu kutokana na changamoto anayoipitia.

“Bado maamuzi ya mwisho hayajafanywa, lakini Ayoub ana wakati mgumu zaidi kwa sababu licha ya kuwa majeruhi, bado akipona atatakiwa kufanya kazi kubwa mazoezini kurejesha utimamu wa mwili, kuna uwezekano mkubwa yeye akaachwa,” alisema mtoa taarifa huyo.

Alisema Fred haonekani kupewa kipaumbele sana na kocha Fadlu, lakini takwimu zake kwenye mechi chache za Ligi Kuu alizocheza msimu uliopita zinampa nafasi ya kubaki mbele ya Lakred.

Msimu uliopita Fred aliingia kwenye timu wakati wa dirisha dogo na kufanikiwa kufunga mabao saba licha ya mara kwa mara kutokea benchi.

**Michezo**

Jumatano Agosti 14, 2024

Nipashe

## Vinicius Jr akataa ofa kutua Saudia

UKURASA 21



# Mambo yawageukia Magoma, mwenzake

●●●Wakamatwa na polisi kwa tuhuma za kughushi saini na kua...



**Adam Fungamwango na Faustine Feliciane**

SIKU chache baada ya kushindwa kesi aliyoifungua dhidi ya uongozi wa klabu ya Yanga, mwanachama maarufu wa klabu hiyo, Juma Ally, maarufu Magoma na mwenzake Geofrey Mwaipopo walikamatwa jana na polisi jijini Dar es Salaam kwa tuhuma za kughushi saini za baadhi ya wadhamini wa klabu hiyo.

Wakili upande wa Magoma na Mwaipopo, Jocob Mashenene, alithibitisha hilo, huku akidai kuwa walikamatwa kwa masuala ya kughushi saini za baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wadhamini, ambao ni mama Fatma Karume na Jabir Katundu.

Masenene alisema wateja wake walikamatwa baada ya kutoka Mahakama Kuu, kusikiliza kesi ya rufani yao dhidi ya Bodi ya Wadhamini wa klabu hiyo ambayo imeahirishwa hadi Agosti 21, mwaka huu.

"Kosa hilo linadhaminiwa na wateja wangu wamekamilisha taratibu zote za kupata dhamana," alisema wakili huyo.

Kukamatwa kwa Magoma na Mwaipopo ni sehemu ya maazimio yaliyofanywa na klabu ya Yanga, kupitia Mwanasheria wake, Simon Patrick, ambaye pamoja na mambo mengine aliahidi kulishughulikia suala hilo akidai kuwa baadhi ya saini ziligushiwa.

"Klabu imetuma maombi ya kupitia upya kesi hiyo kwa sababu hatukushirikishwa na walalamikaji hawakuwa na uhalali wowote, vile vile walifanya kosa la jinai kughushi sahihi za viongozi wakubwa wa klabu tunaamini mahakama itatutendea haki,"alisema Simon kwenye mkutano na waandishi wa habari baada ya mahakamu kutengua uamuzi wa awali katika kesi iliyowapa ushindi Magoma na wenzake.

Magoma na wenzake walifungua kesi Novemba mwaka 2022 wakipinga uongozi uliopo madarakani, kulifuta baraza la wadhamini wa Yanga na kutaka wakabidhiwe timu na mali zote za klabu ili waendeshe wao.

Juni 10, mwaka huu klabu ilipata taarifa hiyo, hivyo uongozi ulituma jopo la mawakili akiwamo Simon kufuatilia suala hilo kwa undani.

**Uongozi wa Yanga pamoja na mawakili wao uligundua kuwa kesi iliyoendeshwa dhidi ya Baraza la Wadhamini ili kuwa ya upande mmoja, huku upande huo huo ukijigawa na kujifanya wengine kuwa upande wa walalamikiwa na kufani kiwa. Lakini uongozi kupi tia wakili Simon uliomba mahakama kufanya upya mapitio ya kesi hiyo kwa sababu awali hawakush irikishwa na jambo am balo lilikubaliwa na ma hakama.**

Wakati huo huo, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi, kuelekea kwenye mchezo wao wa hatua ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, amesema hatowadharau wapinzani wao Vital'O ya Burundi licha ya michezo yote kufanyika hapa nchini.

INAENDELEA UK. 23



Mshambuliaji mpya wa Simba, Leonel Ateba, alipokuwa kwenye majukumu ya kuitumikia Timu ya Taifa ya Cameroon. **PICHA: MTANDAO**

# Rekodi za nyota mpya Simba

**Na Faustine Feliciane**

KLABU ya Simba imetangaza kukamilisha usajili wa mshambuliaji raia wa Cameroon, Lionel Ateba kwa kumsainisha mkataba wa miaka mitatu.

Nyota huyo kutoka klabu ya USM Alger ya Algeria anajiunga na Simba kuongeza nguvu kwenye safu ya ushambuliaji huku viongozi wa timu hiyo wakitakiwa kukata jina moja kwenye orodha ya wachezaji wa kigeni.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema mchezaji huyo amekuja kuongeza makali kwenye kikosi chao kuelekea kwenye Ligi Kuu na mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Hata hivyo rekodi za hivi karibuni za nyota huyo bado hazijahakisi kile ambacho Simba inakihitaji ndani ya klabu hiyo.

Nyota huyo alijiunga na USM Alger, Januari mwaka huu ambapo amecheza michezo 12 ya Ligi Kuu akitumia dakika 754 na kufunga bao moja huku akisaidia

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >